

JE! MUNGU HABADILISHA NIA YAKE KUHUSU NENO LAKE?

 Na tuinamishe vichwa vyetu. Bwana Yesu mpenzi, tumekusanyika tena katika Jina Lako, tukiwa na matumaini makubwa kwa ajili ya kumwagwa kwa Nguvu za kuhuisha za Mungu kutufanya tutambue hali na mahali petu, na jukumu letu, kama watu walioitwa, waliotengwa na ulimwengu, wakawekwa wakfu kwa Mungu. Tujalie, Bwana, usiku wa leo, ili kwamba baraka za Mungu zitatuongoza na kutuelekeza katika mambo tufanyayo ama tusemayo, yapate kuleta heshimna na utukufu kwa Jina Lako. Amina.

² Nina furaha kurudi kanisani usiku huu na kuwa nanyi watu wapenzi. Nami najua kuna joto, bali hivi punde nimempigia simu mke wangu; nafikiri ni tisini na kitu kule, tisini na tano ama tisini na sita ama cho chote kile, na ni joto sana kuliko ilivyo huku. Kwa hiyo ninazoea hali ya hewa yenye joto sasa. Kwa hiyo, bali ninafurahi sana kuwa hapa Maskanini katika wakati huu upendezao sana wa Pasaka.

³ Nami siwezi kusema ya kwamba nitaomba msamaha kwa ajili ya Ujumbe huo mrefu sana, sana asubuhi hii, bali mimi. . . Ulikuwa, sikutaka—sikutaka kuwachosha kisha nije usiku niuhubiri tena. Bali ni—nilitaka ku—kuwaleeteni huo Ujumbe, kwamba ninyi ni sehemu ya ufufuo huu. Mnaona? Na msiufadhaikie Huo, tena, mnaona. Ufurahieni tu! Hakuna kitu, mahali po pote, kinachoweza kuwatenga Nao; hakuna kitu cho chote; mu salama milele katika Ufalme wa Mungu. Wakati Mungu amekupiga Muhuri Yake, wewe ni salama mpaka kwenye mwisho wa safari yako.

⁴ Serikali inapotia muhuri juu ya furushi, idara ya reli ikitia muhuri mlangoni, behewa hilo haliwezi kuguswa hata litakapofika mwisho wa safari yake.

Mungu anapoutia Muhuri Wake juu ya mtu fulani. Na Muhuri hiyo ni Roho Mtakatifu. Anapomtia muhuri mtu namna hiyo, yeye tayari ameenda kwenye kikomo chake cha Milele. Naye hawezi kamwe, kamwe kurudi nyuma tena. Maana kumbukeni, Waefeso 4:30 inasema, “Msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri daima.” Mnaona? Mmetiwa muhuri milele. Mmetiwa muhuri, Milele, katika Ufalme wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu. Sasa wazieni jambo hilo!

⁵ Basi, wewe, ibilisi atakutupia ngumi, na atakwambia kila kitu, na kukushtaki, na—na kujaribu kukufanya wewe ufikiri ya kwamba wewe siye. Bali usimsikilize.

⁶ Sasa, unajua umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Unajua mambo ambayo wakati mmoja uliyapenda, huyapendi tena. Unajua ya kwamba umeamini kila Neno la Mungu. Umemwona Mungu akifanya kazi papa hapa miongoni mwetu, bila ya... Thibitisho lisiloweza kukosa ya kwamba Yeye ndiye “MIMI NIKO” aliye mkuu. Umeona ya kwamba lo lote ambalo limepata kusemwa katika Jina Lake, hakuna jambo moja lililopata kutabiriwa katika Jina Lake ila lililotukia jinsi hasa lilivyotabiriwa. Hata kwa sayansi, gazeti, picha, kamera, waandishi, cho chote kile, hakina budi kutambua jambo hilo. Mnaona, haidhuru kama wanataka ama hawataki, Mungu huwafanya wafanye jambo hilo, hata hivyo, mnaona, kulifanya lijulikane.

⁷ Sasa, tukiwa kundi dogo. Kumbukeni, Yeye haji kwa ajili ya kundi kubwa. “Msiogope, enyi kundi dogo; ni mapenzi ya Baba yenu yaliyo mema...” Mnaona?

⁸ Nataka kuwaachieni neno fulani, la kushtusha, kabla tu ya kuwekwa wakfu kwa muhudumu. Na jambo hili linashtusha sana, lakini ili kwamba mpate kujua. Sasa, mimi sisemi hii ndiyo hesabu kamili, bali ningetaka kuwaachieni jambo hili.

⁹ Sijui kama mtu ye yote hapa ameshawahi kuona kwa kuchanganya mbegu kwa ng’ombe. Jambo ambalo mimi silikubali, siliamini, bali nimeangalia likifanywa. Nami nimewaona wakichukua shahawa ya dume, ya kutosha tu kuwekwa juu ya chuma kidogo, kama kijiti kidogo cha kuchokoa meno, na kuiweka juu ya kipande cha marmar. Na kuweka hizo darubini ambazo huikuza, sijui ni mara ngapi, hata hiyo shahawa... Ambapo usingeweza kuona cho chote kwa jicho lako la kawaida, darubini yo yote ya kawaida. Bali wakati imekuzwa, mara mia moja ama mara mia moja na hamsini, unaweza kuona katika tone hilo moja dogo, la shahawa, labda vijidudu vidogo hamsini mpaka mia moja vikirukaruka kila mahali. Pia, katika ya kike kunatoka mayai mengi, katika—katika shahawa. Sasa, wakati vina—vinapokutanishwa, sasa, vya kwanza viwili ambavyo vinakutana na kuungana...

¹⁰ Kuna kimoja tu kutoka kwenye hivyo milioni moja kitakachoishi. Je! mlipata kuwazia jambo hilo? Ni viini vile vile, na yai lile lile, vyote viwili vinafanana tu, bali kuna kimoja tu kitakachoishi. Na hiyo si kuamua ni kipi kitakachofika pale kwanza. Kwa maana, wakati mwingine yai, lililo kule nyuma kabisa, na ile chembechembe huenda ikawa huko katikati ya shahawa, nazo zitatambaana. Itahitaji Akili Fulani kujua kama itakuwa ni mvulana ama msichana, mwenye nywele nyekundu, nywele nyeusi, ama cho chote kile. Ni kuchagua kwa Mungu. Haiwezi kuwa ni kitu kingine. Kuchaguliwa!

¹¹ Hata katika uzazi wa kawaida, ni kuteuliwa, iwapo itakuwa ni mvulana ama msichana, ama cho chote itakachokuwa. Basi

wakati kijidudu hicho kidogo kinapojongea kikaingia kwenye yai hili dogo, na ile mikia midogo inaanguka, unaanzisha uti wa mgongo wa mtoto mchanga wa cho chote unachotaka; mnyama, mtoto mchanga, ama cho chote kile. Na viini hivyo vingine milioni moja... Mayai milioni moja, vijidudu milioni moja, na ni kimoja tu kinachoishi. Haidhuru, lakini Mungu huchagua kwa kuteua kile kitakachoishi, na vingine vyote vinaangamia. Kimoja katika milioni moja!

¹² Wakati Israeli walipoondoka Misri, wote waliamini katika ujumbe wa nabii mmoja. Waliona ishara za Mungu, kwa njia ya Musa. Kila mmoja wao alizona. Na kila mmoja wao akatoka Misri, na kutembea wakavuka Bahari Ya Shamu, na wakabatizwa katika Musa. Kila mmoja aliona Nguvu za Mungu zikimgusa, alipoimba katika Roho; na wakati Miriamu alipocheza tari, wakakimbia huko na huko pwani. Kila mmoja wao, kila usiku, alikula mana mpya ya kimbinguni itokayo mbinguni. Kila mmoja wa hao alinywea Mwamba ule wa Roho ambao ulikuwa umepigwa. Na kulikuwa na watu milioni mbili waliotoka Misri. Ni wangapi waliofika kwenye nchi ya ahadi? Wawili. Mmoja katika milioni! Wote wako wapi? Yesu alisema waliangamia. “Baba zenu walikula mana jangwani, kwa muda wa miaka thelathini, nami nawaambieni, ya kwamba wote wamekufa.”

¹³ Sasa kuna kama Wakristo milioni mia tano ulimwenguni usiku wa leo, tukihasabu Katoliki, Protestanti, na wote hao. Kama Yesu angekuja katika kule Kunyakuliwa, kulingana na yale niliyosema sasa hivi, kungekuwa na kama mia tano watakaokosekana ulimwenguni usiku huu, katika Kunyakuliwa. Na labda wako hao kila siku, tukihasabu nchi zote, ambao hawajulikani waliko kamwe. Kwa hiyo inaweza kuwa wakati wo wote, mnaona?

¹⁴ Loo, enyi Wakristo, na tujifunge silaha za Mungu. Hebu na tufanye yote tujuayo jinsi ya kufanya, kumtumikia Yeye, kumpenda, na tuongojee wakati huo ulio mkuu.

¹⁵ Sasa, hakutakuweko na milioni nyingi na halaiki ya watu watakaotoka kwenye kizazi kimoja na waingie ndani. Ha—haiwezekani.

Sasa, kumbuka, kila siku humaliza kizazi fulani, kila siku. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji.” Bali kila siku humaliza kipindi fulani cha miaka arobaini kwa mtu fulani, kwa wengine. Mnaona? Na kila siku, kiasi fulani wanatiwa Muhuri katika ule Ufalme. Siku moja, ile siku ya mwisho itafika.

Hebu na tuwe na hakika sasa, tunapokuwa katika akili zetu timamu. Na katika kanisa, na miongoni mwa watu, ambapo Roho Mtakatifu amekwishajitambulisha sana kwetu, hebu na

tuwe na hakika kwamba kila kitu ni sawa, na kinakaa sawa, mbele Zake.

¹⁶ Usikome. Usipumzike, usiku na mchana, mpaka hiyo Nguvu ya Kuhuisha imekuleta kutoka kwenye mambo ya ulimwengu, ikakuingiza katika Ufalme wa Mungu. Nanyi ambao kweli mmeingizwa katika Ufalme wa Mungu na kuhuishwa na Roho wa Mungu, ni furaha jinsi gani! Kwa majoji ya furaha tunapaswa kuwa magotini mwetu, usiku na mchana, tukimshukuru Mungu kwa yale aliyofanya.

¹⁷ Usiku wa leo tuna badiliko dogo katika ibada. Tuna ndugu mzuri hapa, Ndugu Capps. Amekuja kwetu kutoka kanisa la Nazarayo. Nami nafikiri hiyo ni kweli, Ndugu Capps? Yeye anatumata sisi tumweke wakfu usiku wa leo, kwa kumwekea mikono.

¹⁸ Hatuna makaratasi ya kumpa mtu ye yote, hata hivyo tunatambulikana kama . . . Tungeweza kuwa na makaratasi, bali tunaamini ya kwamba mhudumu wa kweli, aliyewekwa wakfu, makaratasi yake yako Mbinguni. Mnaona? Naye—yeye ana haki ya kuihubiri Biblia mradi tu Mungu anayatambulisha maisha yake kwa Biblia. Tunaamini hiyo ndiyo hati yake.

¹⁹ Na, sasa, Ndugu Capps amewekwa wakfu rasmi katika—katika kanisa la Nazarayo, bali usiku wa leo anataka wazee, na kadhalika, wamwekelee mikono kwa kuwekwa wakfu, kuchukua Ujumbe huu. Ni jambo la kishujaa jinsi gani!

²⁰ Nime—nimesikia taarifa tangu nilipokuwa Tucson, na ni ripoti nzuri sana, ya Ndugu Capps hapa katika kumsaidia Ndugu yetu mpendwa Neville, ambaye anashikilia Nuru ya mshumaa kishujaa tu kama watu hawa wawili wanavyoweza kuishikilia. Tumemwekelea mikono Ndugu Neville, bali hatujamwekea Ndugu Capps. Nami nataka wale ambao ni wahudumu, Ndugu Jackson na wengineo, kama wako hapa, na Ndugu Ruddell na wazee wa kanisa hapa, kama watakuja hapa kwa dakika chache tu sasa, na kumwekelea mikono Ndugu Capps. Na ninii . . .

²¹ Sasa tunaona, katika Biblia, ya kwamba hivyo ndivyo walivyofanya jambo hilo, waliwawekea mikono na kuwatenga siku hizo. Na hivyo ndivyo walimfanyia Timotheo. Kasema, “Kwa kipawa hiki kilichokuwa ndani yako, kutoka kwa bibi yako Lois. . .” Walikuwa wamekwisha kuona jambo hilo, ya kwamba kulikuweco na kipawa ndani ya huyo mtu, kilichomjia kwa wazee, kwa kuwekewa mikono.

²² Sasa, ndugu wa siku za baadaye, ndugu wa mvua ya siku za baadaye, walipata, hata hivyo, kuchanganyikiwa na jambo hilo. Wao walifikiri walimpa kipawa, kwa kufanya jambo hilo. La, kile kipawa kilikuwa tayari kimo ndani yake, nao waliweka mikono yao juu yake tu kama idhini ya kwamba waliamini ya kwamba Mungu alikuwa tayari amekiweka hicho kipawa ndani yake. Nao wakakiidhinisha, kwa kuwekea mikono.

²³ Na watu hawa hapa katika kanisa hili, ambao naamini ya kwamba wana Nguvu hii ya Kuhuisha nafsi mwao; kama ninyi ndugu mtakuja humu sasa hivi, Ndugu Ruddell na wengine wenu mlio humu kanisani, na wazee na makanisa mashirika yaliyo karibu, kumwekea mikono Ndugu Capps, ili kwamba apate kuwekwa wakfu kwa kibali chetu, mbele ya wasikilizaji hawa, na kutumwa nje kuhubiri Injili ya Bwana Yesu, po pote Mungu amwitapo. Yeye anakuwa . . .

Yeye tayari ni mmoja wetu, kwa Kuzaliwa. Yeye ni mmoja wetu kwa sababu amekwisha kuamini Ujumbe. Ni mmoja wetu kwa kuwa—kwa kuwa yeye anaitetea Kweli ya Neno. Nasi tunataka Ndugu Capps awekwe wakfu rasmi, mbele yenu, kwa kuwekea mikono, ya kwamba yeye ni mmoja wetu.

Sawa, Ndugu Ruddell, Ndugu Capps, Ndugu Neville. Ndugu Junior Jackson, ye yote wa hao wahudumu wengine hapa, sijui tu ni wangapi waliopo. Sijui . . . Nafikiri wana ibada zao wenyewe usiku wa leo. Kwa hiyo njoni moja kwa moja hapa, Ndugu Capps.

Sasa yuko wapi Ndugu Hunter na hao wengine kutoka New York, mimi . . . Ndugu Anthony? Nafikiri wamerudi. [Ndugu Neville anasema, “Yule kule nyuma Ndugu Anthony.”—Mh.]

Ye yote wenu ninyi wengine mlioko hapa, aliye pamoja nasi, mbona, tungefurahia ninyi kuja hapa na kusimama pamoja nasi sasa, kama kutambua ya kwamba tunaamini Ndugu Capps ndivyo alivyo.

Ni wangapi wenu hapa mnamjua Ndugu Capps, inua mkono wako. Vema, shusha mkono wako chini. Ni wangapi wanaamini ya kwamba yeye ni mtumishi wa Mungu, inueni mikono yenu. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tunampenda, kama ndugu yetu.

²⁴ Sasa hii siyo njia halisi ya kile ambacho tungeita kuweka wakfu, bali nataka wasikilizaji hawa . . . Nisingeweza kuuimba wimbo huu, bali nawatakeni mnisaidie kuuimba. Ule . . .

²⁵ Siku moja nabii mmoja alishuka akaenda madhabahuni, hekaluni. Basi alipokuwa kule hekaluni . . . Yeye alikuwa mtu mzuri, bali alikuwa tu ameegemea mikononi mwa mfalme Uzia, naye alikuwa m—alikuwa mtu mzuri. Bali hata hivyo, siku moja, kule hekaluni, aliona kitu fulani, wakati alipoingia katika ono, ambacho hajapata kukiona hapo awali. Aliwaona Malaika, wenye mabawa, wakiruka huko na huko, humo jengoni, wanalia, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi! Njoni, Ndugu. Naam. Mnaona? “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi!” Ben . . . Unaona?

²⁶ Basi wakati alipofanya hivyo, vizingiti vya hekalu vikatikisika. Ndipo akasema, “Ole wangu! kwa maana mimi ni mtu mwenye midomo michafu.” Katika uwepo wa Mungu

akatambua, ya kwamba hata ingawa alikuwa nabii, alikuwa amekosea. Akasema, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu.”

²⁷ Kisha mmoja wa wale Malaika akaruka, akatwaa kaa la moto akakigusa kinywa chake, akasema, “Tabiri, mwana wa Adamu.”

Waweza kutupa sauti yake, dada, tafadhali. Ni wangapi wanaoujua wimbo huu? Hebu, aya moja. Vema.

Kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,
Likimfanya msafi sana iwezekanavyo,
Sauti ya Mungu iliposema, “Tumtume nani?”
Ndipo akajibu, “Mimi hapa, nitume mimi.”

[Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.]... nena,

Bwana wangu,
Nena, nami nitakujibu Wewe upesi;
Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume.”

Mamilioni sasa katika dhambi na aibu
wanakufa;

Sikiliza kilio chao cha huzuni na cha uchungu;
Hima, ndugu, hima ukawaokoe;
Jibu upesi, “Bwana, mimi hapa.”

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitakujibu Wewe upesi;
Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

Hebu Wazee wazunguke sasa wamwekee mikono Ndugu Capps. Sote na tuinamishe vichwa vyetu.

²⁸ Mungu mpenzi, vizingiti vya hekalu vimetikisika tena, na kwa kuona Roho wa Uzima unayehuisa akitenda kazi katika ndugu yetu. Naomba, Mungu, anaposikia kitu hiki kutoka Juu, ambacho kinasema hana budi kwenda. Tunaweka mikono juu yake, kama wazee Wako, Bwana, na kumpa mkono wa kuume wa ushirika; na kuweka mikono yetu juu yake, na kuruhusu baraka za Mungu juu yake, ya kwamba utatia mafuta midomo yake, mawazo yake, utu wake wote. Na aupeleke Ujumbe huu wa Injili kwenye kila ufa na kona utakayomwita. Jalia hilo, Bwana. Tunakupa Wewe ndugu yetu, kama mtumishi Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁹ “Lihubiri Neno,” ndugu yangu kijana. “Uwe tayari katika wakati ukufaa, na wakati usiokufaa; karipia, kemea, kwa uvumilivu wote na Mafundisho. Mungu akubariki, ndugu.

³⁰ [Ndugu Ben Bryant anasema, “Ndugu Branham, naomba uniwekee mikono tafadhali? Wao wanaweza kuniwekea mikono tafadhali? Ningetaka kuwekwa wakfu.”—Mh.] Wewe ume-... Sikujua hukuwa umewekwa wakfu.

Ndugu Ben, hapa, ametujia. Nafikiri amekuwa akihubiri kwa kitambo fulani. Hata hivyo, bado hajawekwa wakfu (nilifikiri alikuwa amewekwa; hiyo ndiyo sababu nilimwita hapa) rasmi, ama kuwekewa mikono hapa.

³¹ Sasa, mke wa Ndugu Ben yuko hapa mahali fulani, naye ni mtu mwema sana. Alikuwa mhubiri mwanamke. Na wakati yeye na ndugu yetu walipofunga ndoa, naye akamleta Maskanini, wakati alipoona na kulisikia Neno, hata hivyo maskini bibi mzuri akiwa mtu wa tabia nzuri, lakini alipoona ya kwamba ilikuwa ni vibaya kwa wanawake kufanya jambo hilo, alikaa kando; na ilionekana kama jambo hilo linamwangukia mumewe. Hilo ni sawa. Hilo ni kimitume. Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa.

³² Ndugu Ben huzichukua kanda, kama ninavyofahamu, pamoja na mkewe. Wanaenda kwenye ninii. . . mahali pa mbali sana, huko nyuma kabisa milimani, misituni, nao wanazicheza tu kanda hizi na kuzifafanua kanda. Mara nyingi wao wanafukuzwa, wanafukuzwa nje, wanatolewa nje. Tunatazamia mambo hayo. “Kwa maana wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa.”

³³ Ni wangapi hapa wanaomjua Ndugu Ben? Ni wangapi wanaamini yeye ni mtumishi wa Mungu, [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] anayestahili baraka hii ambayo tutamwombea Mungu? Mnaona, yeye si mgeni. Amekuwa pamoja nasi kwa miaka kadha wa kadha. Ninamjua kama mtu mnyenyekevu. Yeye ni kama mimi; anafanya makosa mengi. Sote tunafanya jambo hilo. Kile ninachopenda kuhusu Ndugu Ben, yeye yuko tayari kutambaa kwa magoti yake kulisahihisha.

Basi aliposikia, juzijuzi, juu ya *Ndoa Na Talaka*, yeye na mkewe walikuwa tayari kutengana, kwa maana yeye anampenda, naye mkewe anampenda, bali wao wanataka kuambatana na Neno la Mungu. Lo lote Neno lililosema, hilo ndilo walilotaka. Naomba ya kwamba Mungu atambariki Ben pamoja na mkewe, kwa utumishi Wake.

Na tuiweke mikono yetu juu ya ndugu yetu.

³⁴ Mungu mpenzi, tunaiweka mikono yetu juu ya Ndugu yetu Ben, kwa ishara ya kwamba tunampenda. Nasi tunaamini, Bwana, ya kwamba yeye yu tayari kukufanyia Wewe kazi, kutumwa na hizi kanda, akazicheze kati ya baadhi ya watu wa milimani katika sehemu za mbali sana ambako labda wengi wetu tusingeweza kamwe kufika, bali hata hivyo Ujumbe hauna budi kupelekwa kila mahali ulimwenguni. Tunaomba ya kwamba utambariki ndugu yetu, na umpe Roho Wako, na aje juu yake. Pia umwongoze, na kumwelekeza yeye na mke wake kwenye sehemu zile ambazo labda huyo mtu mmoja yuko huko mbali sana, na milango haiwezi kufungwa mpaka kondoo huyo mmoja ameingizwa. Wewe huridhiki na tisini na tisa. Lile... Kila

jina ambalo limo kwenye kile Kitabu halina budi kuingizwa. Wasaidie, Bwana, tunapoweka mikono yetu juu yake, kama kumshirikisha pamoja nasi kama ndugu yetu. Na msaada wetu na maombi yetu kwa ajili yake, yataambatana naye. Nasi tunaomba ya kwamba utambariki, Bwana, po pote aendapo. Katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, Ndugu Ben! Mkono wa kuume wa ushirika tunakupa, kama ndugu wahudumu. Mungu akubariki, ndugu.

³⁵ [Brother Earl Martin anasema, “Ndugu Branham, waweza kuniwekea mikono tafadhali, kuniweka wakfu nifanye kazi kama mchungaji?”—Mh.] John Martin . . . [“Earl.”] Earl.

Ni wangapi wanaomjua Earl Martin? Ni wangapi wanaoamini yeye ni mtumishi wa Kristo? Yeye anakuja kwetu kutoka . . . Naamini ninii, mwanzoni, kutoka kwenye kundi la Kipentekoste, na sasa nafikiri yeye hufanya kazi ya mchungaji na kufanya kazi ya kujitegemea.

³⁶ Nimemjua Earl kuwa mtumishi halisi wa Kristo. Sitasahau kamwe tendo moja, kumekuweko na mengi, bali tendo moja la Earl. Ninakumbuka usiku mmoja walimwita nilipokuwa Dallas, Texas; ama na—naamini, la, ilikuwa . . . [Dada fulani anasema, “Beaumont.”] Beaumont, Texas, ni kweli, dada. Nao—wao . . . Mtoto wake alikuwa amelala, anakufa, nao walifikiri tayari amekufa. Hakuwa anapumua tena. Ndipo Earl akaja chumbani mwangu, kama baba, mabega yameinama, akainama mbele zangu, kwa kuwa nilikuwa kitandani. Nikatoka kitandani; akanikumbatia kwa mikono yake na kusema, “Ndugu, ninaamini wewe ni nabii wa Mungu. Daima nimeamini jambo hilo. Basi kama tu ukisema neno, ingawa mtoto wangu mchanga amekufa, hata hivyo ataishi.” Ndipo mtoto wake akafufuka, yu hai.

³⁷ Mnaamini yeye anastahili mkono wa kuume wa ushirika wa waumini hawa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Na tuombe, ndugu, tunapoweka mikono juu yake.

³⁸ Baba wa Mbinguni mwenye rehema, tunaiweka mikono yetu, tena, juu ya Ndugu yetu Martin. Tunamtuma, Bwana, kwenye pande za mwisho ambako Wewe umekusudia kwamba anapaswa aende; po pote pale, wengi ama wachache, njia ndogo, njia kubwa, maboma, po pote pale. Hata iwe ni wapi, Bwana, baraka Zako na ziwe pamoja naye. Tunaweka mikono yetu juu yake tunapomwaga na kumpa baraka zetu, ili kwamba Roho aliye juu yetu, Bwana, aende pamoja naye, na atamwongoza na kumwelekeza kwenye nafsi zilizopotea kule nje kwenye maboma na njia kuu. Tunamtuma, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, Ndugu Martin. Nenda sasa, na Bwana awe pamoja nawe.

39 Kwa kusudi lile lile? [Ndugu Richard Blair anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Jina lako ni Richard? [“Naam. Richard Blair.”] Ni wangapi wanamjua Ndugu Richard Blair? Ni wangapi wanaoamini yeye ni mtumishi wa Mungu? Anatoka kwenye ku—kundi la kanisa la United Pentekoste.

Na ndugu, Ndugu Blair, ninaukumbuka mwito mkuu wake. Ninaukumbuka wakati ambapo Ndugu Blair asingeninii, hakutaka kuniamini mimi, kwa sababu kulikuwako na roho fulani aliyekuwa akitenda kazi pamoja naye, akimwambia ya kwamba nilikuwa wa uongo. Basi wakati alipokuwa ameketi papo hapo mkutanoni, Roho Mtakatifu aligeuka na kutamka jambo hilo. [Ndugu Blair anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Naye alikuwa tayari tu karibu ku—kuzimia, huko ndiko kulimfanya awe katika hali hiyo.

Nami nakumbuka mke wake anayependeza akinipigia simu siku moja. Akasema, “Ndugu Branham, ninaamini Richard atakufa.” Naye alikuwa, naamini, na shali. Akaenda akaiweka juu yake, kama nilivyomwambia, na kuomba. Huyu hapa. [Ndugu Blair anasema, “Amina.”—Mh.]

40 Mtoto mchanga alikuwa amepata ajali, ama . . . [Ndugu Blair anasema, “Mvulana wangu.”—Mh.] Mvulana wake, katika ajali, kwamba hawakumwekea sana matumaini, akiwa amezirai kwa mtikiso wa ubongo. Na kwa maombi, hata kwenye simu, mtoto huyo mchanga alipona. [“Amina.”]

Mnaamini ya kwamba Ndugu Blair ni shahidi wa kweli wa Kristo? [Kusanyiko linasema “Amina.”—Mh.] Ombeni ya kwamba baraka zenu ziambatane naye.

Ndugu, wekeni mikono yenu juu yake.

41 Mungu mpenzi, kumtambulisha ndugu yetu mwenye rehema na mwema, mtumishi Wako, ambaye hata amekuja kutoka kwenye kundi lake, kutembea katika Nuru. Baba, tunaomba ya kwamba utambariki Ndugu yetu Blair, tunapomtuma na baraka zetu na kibali chetu, kwa mikono yetu juu yake, kuelekea po pote utakakomwita, Bwana, kwenye kazi yo yote ile. Roho Yako na aambatane na Ndugu Blair. Mwongoze na umwelekeze kwenye waliopotea na wanaokufa wa ulimwengu huu, ili kwamba asaidie kumpata kondoo yule aliyepotea, apate kumrudisha kwenye kundi. Po pote pale, cho chote ulicho nacho kwa ajili yake, Bwana, tunaomba tu ya kwamba Roho Wako amwongoze na amwelekeze wakati wote katika safari ya maisha yake. Sisi ni ndugu zake. Katika kumpa mkono wa kuume wa ushirika, tunakuomba Wewe uambatane naye, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mkono wa kuume wa ushirika! Mungu akubariki, Ndugu Blair. Tuko pamoja nawe, asilimia mia moja, tutakuomba na tutafanya lo lote tuwezalo kukusaidia safarini. Mungu akubariki.

⁴² [Ndugu Merlin Anthon says, “Na mimi vile vile, Ndugu Branham, kuwekwa wakfu.”—Mh.] Ati nini? [Kuwekwa wakfu.”] Jina lako ni nani?” [Merlin Anthon.”] Merlin Anthon. [“Mimi ni wa kanisa.”] Wapi? [“Hapa kanisani.”] Kanisani. Kuna mtu anayemjua Ndugu Merlin Anthon? Yeye ni mgeni, kwangu. [“Pamoja na Jeshi la Wokovu. Wanikumbuka?”] Loo, ndiyo. Samahani, ndugu.

Kutoka Jeshi la Wokovu, hiyo ni kweli, ninamkumbuka. Kweli, ninamjua sasa. Nilininii tu...Sikuona kama ninafahaamu sura yake wakati huo, wakati huu. Ni wangapi wanamjua kuwa ni mtu wa Mungu? [Kusanyiko, “Amina.”—mh.] Ni wangapi wanaamini ya kwamba—ya kwamba Mungu anafanya kazi pamoja naye, inua mkono wako. [“Amina.”] Mtamwombea? [“Amina.”]

⁴³ Sasa, ndugu, tunajua ya kwamba umekuja kutoka kwenye kundi mashuhuri sana la watu, Jeshi la Wokovu, hao ni watu mashuhuri. Lakini, na, lakini Jeshi la Wokovu kweli hufanya kazi kubwa huko nje mitaani. Hatuwezi kusema kitu dhidi ya Nazarayo, kanisa la Kipentekoste, wala Jeshi la Wokovu, wala lo lote lao; hao ni ndugu zetu. Lakini, unaona, tunaamini ya kwamba sisi ni wabebaji wa Ujumbe mkuu wa saa ii hii tunayoishi. Ungetaka kufanya hivyo pamoja nasi? [Ndugu Anthon anasema, “Amina.”—Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu tunapoiweka mikono yetu juu ya ndugu yetu.

⁴⁴ Baba mpenzi wa mbinguni, Wewe Ndiwe unayeita. Wewe Ndiwe unayehuisa Neno, ili kwamba waweze kuamini. Nasi tunaiweka mikono yetu juu ya ndugu yetu mpendwa, kama kibali ya kwamba tunaamini ya kwamba Wewe uko pamoja naye na utamsaidia. Tunatuma baraka zetu pamoja naye, ya kwamba sisi ambao tunaamini ya kwamba tumepita kutoka mautini tukaingia Uzimani na sasa tunashikilia Nguvu za Kuhuisha mioyoni mwetu, kwa neema ya Mungu. Tunaweka mikono juu ya ndugu yetu na kumtuma pamoja na baraka zetu, ya kwamba utamtangulia na kumwonyesha njia na kumwelekeza yeye kwenye kila ufa wa dunia, Bwana, ambako Wewe umekusudia ya kwamba ataenda. Roho Wako na aambatane naye na ampe afya, nguvu, na ufanisi katika huduma yake, kwa maana tunamtuma katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁴⁵ Mungu akubariki, Ndugu. Huo ndio mkono wa kuume wa ushirika, mnajua, ninyi ndugu mpeni mikono, ndugu hawa namna hiyo. Ili kwamba mwe... Vema, Bwana awabariki nyote.

⁴⁶ [Ndugu Carrell anasema, “Si—sijafanyiwa jambo hilo, rasmi. Nataka wewe uweke mikono yako juu yangu, kama hao, katika Jina la Yesu.”—Mh.] Wewe, lo lote unalotaka. Na yenu...[Ni wakati wa kuwekewa, na kama hao.”] Basi jina lako ni nani? [“Ndugu Carrell, kutoka Cincinnati.”] Ndugu Carrell.

[Ndugu Carrell anasema, “Nilikuwa mhudumu aliyewekwa wakfu, bali nisingekubaliana na Ndugu aliyekuwa anawaweka wanawake wakfu kama wahudumu, ndipo ikanibidi kujitenga nalo.”—Mh.]

Huyu ni Ndugu Carrell kutoka Cincinnati. Mtu ye yote anayemjua Ndugu Carrell, inua ninii wako... Kwa kuwa ametoka Cincinnati, nina shaka, ya kwamba kuna mtu anayemjua. Yeye anasema ya kwamba alikuwa na kundi fulani, na kundi hilo lilitaka kuwaweka wakfu wahudumu wanawake. Hakuweza kuvumilia jambo hilo, basi ikambidi kujitenga nalo.

Hivyo ndivyo hasa nilivyojitenga na Batisti ya Kimishenari. Daktari Roy E. Davis, ni wangapi wamewahi kumsikia? Hakika, mlimsikia, mnaona. Alitaka kuwaweka wakfu baadhi ya wahubiri wanawake, nami nikasema, “La, bwana. Kama mzee,” nikasema, “siwezi kufanya jambo hilo, nikijua. Linapingana na Neno la Mungu.”

⁴⁷ Sikujui, Ndugu Carrell. Bali juu ya msingi wa ushuhuda wako, na hiyo Kweli unayoitetea... Hatuna kitu dhidi ya wanawake hao. Hao ni dada. Tunawapenda. Bali tunaamini ya kwamba wana mahali pao, na ya kwamba hawana budi kukaa. Mnaona? Nasi tunaamini ya kwamba wao ni wapenzi kwa mwanamume, msaidizi. Na hawapaswi kabisa... Tunafikiri wao ndio kipawa kikubwa kuliko vyote, nje ya wokovu, ambacho Mungu aliwahi kumpa mwanamume. Bali yeye hana mahali mimbarani, kulingana na Neno la Mungu. Juu ya msingi huo, pamoja na imani yako kwa Mungu, tunaweka mikono juu yako, kama ushirika, uje uende pamoja nasi.

Na tuiweke mikono yetu juu yake.

⁴⁸ Baba yetu Mpenzi wa Mbinguni! Kijana huyu, karibu naweza kujua anavyojisikia. Amefukuzwa kwa ajili ya Kweli halisi. Ya kwamba, “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno.” Kwa hiyo tunamwekea mikono, tukiweka baraka zetu juu yake. Roho Wako na amtangulie, amwonyeshe njia, na amwelekeze kila mahali katika safari ya maisha po pote utakapomtuma, Bwana. Mjalie kujua ya kwamba tunamwombea, nasi tutakuwa msaada kwake, na kumpa moyo mradi tu ataitetea ile Kweli. Tujalie, Bwana. Tunamtuma, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, Ndugu Carrell.

Mnawawekea mikono tu, watu mbalimbali. Ninyi nyote mnatoa mikono ya kulia ya ushirika kwa ajili ya jambo hilo.

⁴⁹ Ndugu Ruddell, hapa, hajawekwa wakfu rasmi hapa kanisani. Mnaweza... Ni wangapi wanamjua Ndugu Ruddell? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sote tunamjua. Ni wangapi wanajua ya kwamba ni mtu wa Mungu? [“Amina.”—Mh.]

Baba mpenzi wa Mbinguni, tukiwa kama wazee Wako tunaweka mikono juu ya ndugu huyu ambaye amepitia kwenye maji ya matope yenye kilindi. Yeye ameona kusanyiko lake likianguka. Ameona kila kitu kikitukia, lakini hata hivyo anaamini. Ingawa ninii...?...Tunaweka mikono yetu juu yake, na kumpa baraka zetu...?...Mtie mafuta, Bwana, kwa nguvu, pamoja na Neno, Bwana, na umtume kwenye kila mwanya wa dunia!...?...uwe pamoja naye na kumsaidia. Na ukamtume, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁵⁰ Ndugu Ruddell, daima una mkono wa kulia wa ushirika. Namjua Ndugu Ruddell. Anaonekana kama—kama mvlana wangu mwenyewe. Mimi na baba yake, mama, tumejuana kwa muda mrefu sana. Nami ninamjua Ndugu Ruddell kuwa mtumishi wa Mungu. Nimetumika pamoja Naye. Mungu akubariki, Ndugu Ruddell.

⁵¹ Jina lako ni nani? Wewe ni nani, ndugu? [Mtu fulani anasema, “Shemeji wa Ndugu Martin.”—Mh.] Ndugu Martin, unamjua, Ndugu Martin?

Jina lako ni nani? [Ndugu huyo anasema, “Kasisi McComas.”—Mh.] Ndugu McComas. Nafikiri hakuna mtu hapa anamjua, bali yeye ni...Naam, mtu huyu hapa anayemjua, Ndugu Tyler. Naye anakuja kuninii...kuwekewa mikono, ili kwamba awe mbebaji wa Injili. Ndugu McComas, umetoka wapi, Ndugu McComas? [“Rockford, Illinois.”] Rockford, Illinois. [Ulipiga simu nyumbani kwangu, juma lililopita, ama usiku wa Jumatatu iliyopita, ukamwomba mke wangu.”] Loo, hiyo ni kweli? Kutoka Tucson. [Tucson, Arizona.”] Loo, ninakumbuka simu hiyo sasa. [“Aliamka asubuhi yake.”] Bwana asifiwe!

[Ndugu Martin anamwambia Ndugu Branham jambo fulani—Mh.] Ati nini? [“Dada yangu mdogo kabisa.”] Dada yako. [“Yuko hapa sasa. Alikuwa amepooza.”] Kwa hiyo, yeye yuko hapa sasa, aliombewa, juzijuzi usiku, kutoka Tucson, kwa simu. [“Amepooza.”] Kupo-...[“Alikuwa amepooza, naye yuko hapa sasa.”] Alikuwa amepooza, siku chache zilizopita usiku, naye yuko hapa sasa. Ndugu Martin wakati huo alikuwa anakuomba. Si ajabu anataka kuupeleka Ujumbe!

Na tumwekee mikono, ndugu.

⁵² Mungu mpenzi, ninaweka mikono, pamoja na hawa wengine, juu ya mtumishi Wako, na kumpa mkono wa kuume wa ushirika, tukiomba ya kwamba baraka za Mungu zita-...?...[Maneno ya Ndugu Branham hayawezi kusikika vizuri—Mh.]...?... uliyomwekea wakfu. Baraka Zako ziwe juu yake, na umwongoze na kumwelekeza, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mkono wa kulia wa ushirika, ndugu yangu, na ya hao iwe pamoja nawe. Mungu awe pamoja nawe.

⁵³ [Mtu fulani anasema, “Ndugu Branham?”—Mh.] Ndio, Ndugu? [“Nina mmoja zaidi anayetaka jambo hili pia.”]

Sawa, bwana. Ninaamini huyu ni...[“Ndugu Darris.”] Ndugu Darris. Sininii...[“Namjua Ndugu Earl na Ndugu Brewer.”] Mtu huyu ni Ndugu Darris. Umetoka wapi, Ndugu? [“Black Rock, Arkansas.”] Black Rock, Arkansas. Ndugu... [“Ninamjua, ndugu.”]...umemjua. Mtu mwingine, ninaamini, hapa, alisema...Ndugu Brewer. Ninaamini nilikutana nao, asubuhi ya leo. Na—na Dada Vayle, nafikiri, Ndugu Vayle, na hao wanaomjua, na wanamjua kuwa ni mtu wa Mungu, mtumishi wa Mungu. Vizuri sana!

⁵⁴ Vema, sasa, ndugu yangu mpendwa, kuwa mbebaji wa Ujumbe, tunataka ujue ya kwamba tunasimama nyuma yako, kufanya kila tuwezacho. Tutakuwa tukikuombea, kwamba wewe pia uubebe Ujumbe huu hadi pande za mwisho po pote pale Mungu alipokuchagua kwenda.

Hebu na tuweke mikono yetu juu ya Ndugu yetu Darris.

Mungu mpendwa, sasa tunaiweka mikono yetu juu ya ndugu yetu, tukimpa mkono wa kuume wa ushirika, na kumtuma katika Jina la Yesu Kristo, ili kwamba umtie mafuta. Na...?... na kumpa mkono wa kuume wa ushirika!...?...Na Roho Wako aambatane naye, na kumwongoza na kumwelekeza, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, ndugu.

⁵⁵ Na—naamini, Ndugu Anthony. Wengi wenu mnamjua Ndugu Anthony. Amekuwa hapa pamoja nasi kwa muda mrefu. Ninamjua kuwa mtumishi wa Kristo, mimi mwenyewe. Ninaamini ni kijana aliyejitolea. Hajawahi kuwekewa mikono rasmi. Yeye hakujua jambo hili lilikuwa linakuja, marafiki. Mnaona? Lakini sasa hivi ni wakati mzuri kama mwingine wote. Kwa hiyo tutaweka mikono yetu juu ya Ndugu Anthony na kumpa tu mkono wa kuume wa ushirika. Mungu hana budi kuweka wakfu. Hii ni kumjulisha tu, nanyi mjue, ya kwamba tunamwamini ndugu huyu na tunampenda, naye ni mmoja wetu, katika Ujumbe. Nasi tunamtaka apate baraka za Mungu, na hizo ndizo tunazomwomba. Hebu na tuombe, tunapoweka mikono yetu juu ya, ndugu.

⁵⁶ Mungu mpenzi, maskini mtumishi huyu Wako Mwitaliano mnyenyekevu, Bwana, anakuja usiku wa leo, ili kwa—kwamba awekewe mikono, na mkono wa kuume wa ushirika, apewe, rasmi, na kanisa. Bwana, Nguvu Zako kuu zikamtume mvulana huyu mdogo kwenye...?...ya dunia na kwenye nyufa ambako umemwitia. Naomba aende na kuwakomboa hao watu kutoka kwenye dhambi na maradhi, na kukutumikia Wewe, Bwana, siku zote za maisha yake. Na umtangulie, umwogoze. Baraka zetu na ziwe juu yake, tunapomtuma, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki.

⁵⁷ [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ati? Loo, sijui. Tunawasiliana kwa simu; senti hamsini kwa dakika moja. Kulikuwa na mtu mwingine hapa aliyetaka . . .

Njoni hapa na msem majina yenu, ninyi ni nani, ndugu, kupitia tu kwa maikrofoni tu moja kwa moja *hapa*. Waambieni tu. [Kila ndugu anataja jina lake mwenyewe, “Pat Tyler,” “Claude Boggess,” “Dale Potter,” “. . . ? . . . Henasey,” “James Humes,” “Earl Horner.—Mh.] Hao ndio? [Mtu fulani anasema, “Ndiyo.”] Ndugu zangu.

Wanaume hawa, mnaamini Ujumbe huu kwamba ni Kweli kutoka kwenye Neno la Mungu? [Hao ndugu wanasema, “Amina.”—Mh.] Mnaamini jambo hilo kwa mioyo yenu yote? [“Amina.”] Vema. Nanyi mna shauku, na mnafikiri kama tukiwawekea mikono . . . Tunataka ninyi mjue ya kwamba tuko pamoja nanyi, nasi tutafanya lo lote tuwezalo kufanya kuwasaidieni.

Na sasa nawatakeni ninyi ndugu, ili kwamba niweze kuweka mikono juu yao, mje moja kwa moja hapa sasa. Nasi sote na tuinamishe vichwa vyetu, tunapowawekea mikono.

Mungu mpenzi, hili hapa kundi la watu. Naiweka mikono yangu juu ya kila mmoja wao, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Na jalia kwamba Wewe, Ambaye umewaita kuwa wahudumu, kwamba na wauhubiri Huo, Bwana, siku zote za maisha yao. Na . . . ? . . . kuhubiri Injili kwa kila kiumbe. Tunawapa hao mkono wa kuume wa ushirika, na kuomba baraka Zako ziwe pamoja nao, Bwana, tunapowabariki, kuwapa baraka zetu. Jalia uende katika kila ufa wa dunia ambako umewaita kwenda. Jalia wakutendee kazi Wewe na kukutumikia katika uweza uliowaitia. Naomba wawe mashujaa na watumishi halisi wa Mungu. Jalia jambo hilo, Bwana. Nasi tunaomba katika Jina la Yesu Kristo.

⁵⁸ Mungu awabariki, kila mmoja, enyi ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki, Ndugu Humes. Mungu awe pamoja nanyi, kila mmoja.

Kibarikiwe kifungo kiifungacho
Mioyo yetu katika Upendo wa Kristo;
Ushirika wa nia moja
Ni kama wa huko Juu.

⁵⁹ Yeye si ni wa ajabu? Wazieni tu sasa, ni wahudumu wangapi walioko hapa usiku huu kusudi wawekewe mikono!

⁶⁰ Sikujua ya kwamba tulikuwa kwenye mawasiliano haya ya simu. Kama watu huko nje watanisamehe kwa jambo hilo; sikujua. Mnaona? Mimi sikujua watautuma kwa simu Ujumbe huu mdogo usiku huu. Lakini sisi tuna- . . .

⁶¹ Sasa tutalisoma Neno na kuomba, na kuingia kwenye Ujumbe huu moja kwa moja ambao najisikia ya kwamba Roho Mtakatifu angenitaka niwalettee usiku huu.

⁶² Na sasa wakati tunapofungua kule nyuma katika...kwa ajili ya somo, nitalitangaza mnamo dakika moja. Hebu tufungue Hesabu, sura ya 22, aya ya 31. Hesabu 22:31, kwa ajili ya somo. Wakati mnapofungua, kama mnataka kusoma, kulisoma ama kuliandika.

⁶³ Nawatakeni nyinyi nyote mnikumbuke sasa, hata nitakapoweza kuwaona tena, natumaini, yapata wakati fulani wa majira haya ya kiangazi, Bwana akipenda. Na kama jambo lo lote likitukia, nisiende katika nchi za ng'ambo, nitarudi. Lakini sasa tunaamini ya kwamba, vile haya yote yamefanikiwa kila mahali, ya kwamba Roho Mtakatifu atatutuma sasa kwenye njia ambayo amejichagulia Mwenyewe kututuma. Na hivyo ndivyo tunavyotaka kutenda jambo hilo. Bwana na awabariki!

⁶⁴ Baba, tuko karibu kusoma Neno Lako. Tafadhali libariki na kulitia mafuta tupate kulifahamu, tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁶⁵ Kitabu cha Hesabu, sura ya 22 na aya ya 31:

Basi ndipo BWANA akafunua macho ya Balaamu, akamwona malaika wa Bwana amesimama njiani, ana upanga mkononi mwake, umekwisha kufutwa; naye akainama kichwa, akaanguka kifudifudi.

⁶⁶ Sasa, katika kusoma hili, kufanya fungu la maneno kwake, nataka kuchukua somo: *Je! Mungu Hubadilisha Nia Yake Kuhusu Neno Lake?*

⁶⁷ Hilo ni somo kweli kweli, nayo ni Kweli kuu ambayo inatupasa kufahamu. Je! Mungu anaweza kusema cho chote kisha aseme, "Samahani nilisema jambo hilo"? Hivi Mungu anaweza kughairi Neno Lake baada ya kulisema?

⁶⁸ Sasa, katika maneno haya hapa, sababu ya mimi kuchagua maneno haya, ilikuwa ni kwa sababu ni moja ya maneno ya Biblia ambayo msomaji, akijaribu kuona, ama kujaribu kusema ya kwamba Mungu hubadilisha nia Yake; hapa ingeonekana zaidi kama kwamba Yeye alibadilisha nia Yake kuliko mahali po pote katika Biblia, nipajuapo, kwa sababu Yeye alimwambia Balaamu jambo moja halafu akamwambia lingine. Na sasa, watu wengi wamejaribu kumfanya Balaamu ninii tu, loo, mnajimu ama kitu fulani. Bali Balaamu hakuwa mnajimu. Yeye alikuwa nabii wa Bwana.

⁶⁹ Sasa, kwa namna fulani tutapata mhitasari wa Ujumbe, kwanza. Israeli walikuwa katika safari yao kutoka Pales... wakielekea Palestina, wakitoka Misri. Naye Bwana alikuwa pamoja nao, nao walikuwa...Kila adui aliyekuwa ameinuka dhidi ya Israeli aliondolewa njiani, kwa maana Mungu alisema

angewapeleka mavu mbele yao na wangemfukuza adui, mradi tu wao walitembea katika utii wa amri Yake. Kazi kamwe haikuwa kubwa kupita kiasi. Waamaleki, hao majitu wa siku hizo, hawakumaanisha kitu kwa Israeli. Ingawa wao walikuwa watu wafupi kwa kimo, bali walikuwa wakitembea katika BWANA ASEMA HIVI. Kwa hiyo haidhuru pingamizi zilikuwa nini, Mungu daima aliona ya kwamba maneno yake ya ahadi hayakuwapungukia Israeli.

⁷⁰ Na Israeli wa Agano la Kale ni mfano wa Bibi-arusi wa Agano Jipya, akiya kutoka u—ulimwenguni, akienda zake Kanaani, ama Kanaani ambayo tunaenda, ule Utawala wa Miaka Elfu.

⁷¹ Basi, sasa, tunaona Moabu hapa ni mfano wa kanisa. Na Moabu. . . Walikuwa ndiyo kwanza wawapige wafalme na kumshinda adui, wakaua kila kitu, wakaitwaa nchi, nao wakasogea karibu na Moabu. Sasa, Moabu bila shaka halikuwa taifa la kikafiri. Moabu lilikuwa taifa lililomtumikia Mungu yule yule waliyemtumikia Israeli. Nayo nchi ya Moabu hapo awali ilianzishwa na mwana wa Lutu, kwa binti yake mwenyewe. Naye, akiwa mwanzilishi wa taifa hili, na alikuwa amewaweka kwenye taratibu watu wake mashuhuri na kadhalika, na kuunda taifa kubwa nao, nao walikuwa wameongezeka na kuendelea.

⁷² Basi, sasa, Israeli walikuwa wa mzao wa Ibrahimu, si wa Lutu. Israeli walitokana na Isaka, Yakobo. Na Israeli walitoka katika hao makabila kumi na mawili yaliyotokana na Yakobo, ambaye baadaye aliitwa “Israeli,” kwa maana alishindana mwereka na Bwana. Na Moabu hapa. . .

⁷³ Sasa, katika jambo hili, nanyi watu huko nje kwenye—kwenye simu, nataka kwanza kusema ya kwamba si—sitaki kutoa lawama, nami natumaini sitoi. Bali, Ujumbe ambao nimepewa mimi, sina budi kuwa mwaminifu kwa Ujumbe huo, la siyo nitakuwa mnafiki. Mnaona? Si—siwezi kusema zaidi ya yale niliyotumwa kusema.

Nami ni—ninafikiri ya kwamba adui mkubwa wa jamii ya Kikristo leo ni makanisa yaliyounda madhehebu. Ninaamini kwa moyo wangu wote ya kwamba hatimaye yatafanyiza ile alama ya mnyama, ambayo naweza, nafikiri naweza kuthibitisha jambo hilo kwa Biblia kwa msaada wa Mungu. Tayari nimefanya jambo hilo. Ya kwamba, yatafanyiza alama ya mnyama, katika muungano wa makanisa. Kwa kuwa, Mungu hajatambua, hata wakati mmoja, makanisa yaliyochaguliwa, yaliyounda madhehebu, la hashu. Yeye hajayatambua kamwe.

Na kila wakati ambapo mwanadamu aliunda madhehebu, Roho wa Mungu aliyaacha wala hakurudi tena. Mwulize mwanahistoria ye yote, ama huenda ukawa msomaji wewe mwenyewe. La hashu! Walipounda madhehebu, Mungu aliyaweka rafuni, na huko ndiko yalikoelekea; yalikokaa, tangu

wakati huo na kuendelea. Wafuasi wao waliongezeka, bali si uamsho wa Roho kamwe; la hasha, hapana tena.

⁷⁴ Moabu, hapa, ni mfano wa hayo, kwa maana wao walikuwa ta—taifa lenye taratibu; katika nchi yao wenyewe, kama vile katika madhehebu yao. Basi huko walikuwa na dini zao wenyewe, na dini yao ilikuwa dini ile ile waliyokuwa nayo Israeli. Wao walikuwa Wamoabu na walimwamini Yehova Mungu, bali wao walikuwa kundi la watu wenye utaratibu.

⁷⁵ Basi, sasa, kama vile wanavyoliwakilisha kanisa la kawaida, Israeli inaliwakilisha kanisa la kiroho katika safari yake. Sasa, Israeli halikuwa taifa lenye utaratibu. Mradi tu walimfuata Mungu, wao walikuwa huru. Walikuja, ni wageni, hawana mahali pa kwenda. Po pote ilipokwenda ile Nguzo ya Moto, wao waliambatana Nayo. Wao hawakuwa taifa lenye utaratibu. Wao walikuwa na utaratibu kati yao, kwa maana tohara iliwapa huo chini ya amri ya Mungu, bali si taifa lenye umadhehebu wakati huu. Wakati hatimaye walifanyika taifa la kimadhehebu, hapo ndipo walipoanguka na kumkataa Masihi wao.

⁷⁶ Basi sasa tunaona, kila mara, ya kwamba wakati roho hizi za rohoni na za kawaida, za makanisa na madhehebu, zinapokutana, daima kuna mgongano. Haijakosa kuwa hivyo. Daima hupambana. Kwa sababu, tunaona ya kwamba mle ndani kuna wivu. Na, katika wivu huu, unasababisha kujilinganisha kimwili, miigo ya kimwili. Nasi tunaona jambo hilo siku hizi, kama ilivyokuwa wakati huo. Mungu anapofanya jambo fulani kwa mtu binafsi, kila mtu hujaribu kuiga tu kama vile Mungu alivyomfanyia mtu huyo. Mnaona, inasababisha mashindano, na inasababisha mambo ya kimwili. Halafu basi kama wao hawawezi, upande ule mwingine, kupata matokeo ya kiroho, basi wanalichukua kwa nguvu za kisiasa, ama wanabadilisha kitu fulani, ili kufadhaisha mioyo ya watu, wapate kuwavuta wanafunzi kwao.

⁷⁷ Hilo ndilo hasa lililotukia pale mwanzo kabisa; kama vile Kaini na Habili, wavulana hao wawili hapa duniani. Na wakati Habili alipomtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini, na Mungu akamthibitisha Habili, kwa kushuka na kupokea dhabihu yake; ilimfanya Kaini aone wivu, kwa maana alimwonea nduguye wivu, kisha akamwua nduguye.

⁷⁸ Ilianzia hapo mwanzo, ambapo wa kimwili na wa kiroho, ingawa Kaini na Habili walimwabudu Mungu yule yule. Wote wawili walijenga madhabahu za namna ile ile. Na wote wawili walimwabudu Mungu yule yule, katika kanisa lile lile, madhabahu yale yale. Lakini Kaini, kwa hoja za kimwili, alileta matunda ya nchi na kuyaweka juu ya madhabau kama dhabihu, akifikiri ya kwamba hakika jambo hili lingemridhisha Mungu kwa ajili ya upatanisho. Kwa hiyo hapana budi alileta, kama vile watu wanavyofikiri leo, “matofaa ambayo Adamu

na Hawa walikula, yaliyosababisha ile dhambi.” Na, cho chote kile, nafikiri sasa wamefikia kwenye “komamanga” ama cho chote kile sasa. Wengine wao walisema, si muda mrefu uliopita, ilikuwa ni kitu kingine.

⁷⁹ Na, ila Habili alikuwa na dhabihu ya kweli. Alijua ya kwamba damu ndiyo iliyosababisha jambo hilo, kwa hiyo akaleta mwana-kondoo. Na wakati Mungu alipopokea ninii yake, sasa, Habili, kwa imani, kwa ufunuo, hakuna njia nyingine. Hapakuwepo na Biblia iliyokuwa imeandikwa. Kwa hiyo, mnaona, chanzo cha haki ni Kweli ya Mungu iliyofunuliwa, na Kanisa zima la Mungu aliye Hai limenjengwa juu ya jambo hilo.

⁸⁰ Yesu, siku moja, akishuka kutoka mlimani, aliwaambia wanafunzi Wake, “Watu hunena Mimi, Mwana wa Adamu, kuwa ni nani?”

Mmoja alisema Wewe ni ‘Musa,’ na mwingine anasema, Wewe ni ‘Eliya,’ na Wewe ni ‘Yeremia,’ ama mmoja wa manabii.”

Yeye akasema, “Nanyi mwaninena Mimi kuwa ni nani?”

⁸¹ Hapo ndipo mtume Petro, akiwa amevuviwa na Mungu, akahuishwa na Roho, alitoa tamshi lile muhimu sana, “Wewe Ndiye Kristo, Mwana wa Mungu aliye Hai.”

⁸² Angalia tamshi hilo. “Heri wewe, Simoni, Bar-Yona, mwili na damu havikukufunulia hili. Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Wewe ndiwe Simoni. Juu ya mwamba huu...”

Mwamba gani? Sasa, Wakatoliki husema, “Juu ya Petro, yule mwamba, jiwe dogo.” Nao Waprotestanti wanasema, “Juu ya Kristo, aliye Mwamba.”

Si kuwa tofauti; bali ilikuwa juu ya ule ufunuo aliokuwa nao Petro, kwamba Yeye alikuwa ni Nani. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu,” kasema Yesu, “asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu.”

“Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye Hai.”

⁸³ “Heri wewe, Simoni, Bar-Yona; mwili na damu havikukufunulia jambo hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni. Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.” Neno la Mungu lililofunuliwa Kiroho!

⁸⁴ Angalia, Habili, kwa imani katika Mungu, alitoa dhabihu iliyo bora. Na mwamini wa kimwili akafikiri ya kwamba ilikuwa ni kazi za mikono yake mwenyewe, ambayo, na matunda yake na dhabihu nzuri aliyoileta, ambayo Mungu angetambua, na jambo hilo likasababisha mgongano.

Tunaona ya kwamba Ibrahimu na Lutu walikuwa na mgongano.

85 Tunaona ya kwamba Musa na—na Dathani, Kora, walikuwa na mgongano ule ule.

Musa, akiwa nabii aliyechaguliwa na Neno la Bwana, alithibitishwa ya kwamba alikuwa amechaguliwa kuwa kiongozi wao kwa ajili ya majira hayo, na ya kwamba Ibrahimu alikuwa ameahidi mambo haya yote, na hapa Musa alifanya kile hasa Mungu alichosema kingekuwa, kingetukia.

Naye Kora, akiwa wa kimwili, alitaka kuinua madhehebu miongoni mwao. Alitaka kuunda kundi la watu. Naye Mungu hashughuliki na watu namna hiyo. Inaonyesha papo hapo, kwenye Maandiko hayo, mfano wa ile safari leo, ya kwamba madhehebu si jambo analochagua Mungu. Kwa maana, mara Kora alipofanya jambo hilo, alimwambia Musa, “Unajichukulia mengi mno juu yako.” Katika maneno mengine, “Kusanyiko lote ni takatifu! Mbona, unasema ya kwamba wewe ndiwe mtu pekee mtakatifu. Huna haki ya kufanya jambo kama hilo. Unajaribu kujifanya mwenyewe mtu fulani mkubwa. Sisi sote tu watakatifu. Sisi sote ni watoto wa Mungu.”

86 Naye Musa aligeuza tu kichwa chake akaondoka. Akasema, “Bwana, nitafanya nini?”

87 Mungu akasema, “Jitenge naye. Nimechoshwa na jambo hilo.” Naye akammeza katika nchi.

88 Mnaona, kulikuwa na mgongano. Wakati wa kimwili na wa kiroho wanapokutana, daima kuna mgongano. Yuda na Yesu walipokutana, kulikuwa na mgongano; Mmoja, Mwana wa Mungu; huyo mwingine, mwana wa Shetani. Kama tu Kaini na Habili, kulikuwako na magongano walipokutana. Mmoja wao alikuwa mweka hazina wa kanisa, na yule Mwingine mchungaji. Na kama ilivyo sasa, tunakuja kwenye siku hizi, kwenye kitu kile kile tena. Madhehebu ya kimwili ukilinganisha na Bibi-Arusi wa kiroho wa Kristo. Bibi-arusi wa kiroho wa Kristo ni tofauti sana na madhehebu ya kimwili, mpaka hakuna cha kulinganishwa kati yao hata kidogo.

89 Sasa angalia, wa kawaida daima hujaribu kujifananisha na wa kiroho. Bali, kama vile katika Yakobo na Esau, hilo halitafaulu. Halingefaulu. Naam, inapofikia kufanya kazi nzuri, na—naamini ya kwamba Esau kweli alikuwa mtu bora kuliko Yakobo, mbele za watu. Yeye alijaribu kumtunza babaye; alikuwa kipofu, nabii. Na mambo haya yote aliyotaribu kufanya, bali hata hivyo Esau hakufikiri kwamba hiyo ni kazi ya kimwili tu. Yeye alifikiri angeweza kuingia kwa yale aliyoyafanya, kufanya jambo fulani zuri kwa ajili ya mtu fulani, ambalo lilikuwa ni sawa. Bali Yakobo, nafsi yake yote ilikuwa ni kupata hiyo haki ya mzaliwa na kwanza, na jambo hilo ndilo Mungu alilotambua ndani yake kwamba ni la kiroho.

90 Angalia, basi jambo hilo daima limemfanya wa kimwili kumchukia wa kiroho. Lilimfanya Kaini kumchukia Habili.

Lilimfanya Kora kumchukia Musa. Lilimfanya Yuda kumchukia Yesu. Na inaendelea na kuendelea. Linamfanya wa kimwili kumchukia wa kiroho, kama vile tu Kaini hapo mwanzo alivyomchukia Habili, yule ambaye Mungu alipokea dhabihu yake, na hujaribu kuwaangamiza.

Hata wao hujaribu kuharibu sifa. Wanajaribu kuharibu kila kitu, kwa sababu si kitu ila wivu. Lilianzia kwa Kaini na ikathibitika kwamba ni wivu, na lingali ni jambo lile lile leo wakati yule wa ulimwengu (wa kimwili) na wa kiroho wanapokutana pamoja. Inathibitisha kwamba ni Shetani, hakuna njia nyingine, kwa kuwa wivu unatokana na Shetani. Halafu jambo hilo linasababisha kuigiza kwa ile Kweli, mtu fulani kujaribu kuigiza kitu ambacho si ninii, wao hawajachaguliwa kufanya. Ni mangapi ya mambo hayo tumeona katika siku hizi za mwisho! Loo, jamani, ni mangapi ya hayo!

⁹¹ Kwa hiyo tunaona Mungu mi...milele habadilishi nia Yake kuhusu Neno Lake la asili. Bali, yule Yeye anayemwita, huyo ndiye anayemchagua. Hakuna mwingine anayeweza kupachukua mahali pale. Hakuna mtu angaliweza kupachukua mahali pa Musa. Haidhuru ni Kora wangapi walioinuka, na ni Dathan wangapi; ilikuwa ni Musa, Mungu alikuwa amemwitwa, kwa vyo vyote.

⁹² Lakini, na iwapo watu hawatatembea katika mapenzi Yake makamilifu, Yeye ana mapenzi ya kuruhusia atakayokufanya uende kwayo. Angalia, Yeye hurusu jambo hilo, kweli, bali atalifanya litende kazi kwa utukufu Wake, katika mapenzi Yake makamilifu. Sasa kama mngetaka...

⁹³ Kama tu, hapo mwanzo, haikuwa ni mapenzi makamilifu ya Mungu kwa watoto kuzaliwa duniani kwa kujuana kimwili. La, bwana. Mungu alimuumba mtu kutoka kwenye mavumbi ya nchi, akampulizia ndani yake pumzi ya uhai, naye akawa nafsi iliyo hai. Alitoa kutoka katika mtu huyo msaidizi, na kumfanyia mke. Hayo yalikuwa mapenzi ya kwanza na ya asili ya Mungu. Bali wakati dhambi ilipoingia na kufanya jambo ililofanya, basi Yeye alimruhusu mwanamume kuoa mke, kisheria, na kupata watoto kwake. "Ongezeken mkaijaze nchi, basi, kama hivyo ndivyo mtakavyofanya jambo hilo." Lakini, mnaona, jambo hilo kamwe halikuwa mapenzi Yake makamilifu.

⁹⁴ Kwa hiyo, mambo haya yote yaliyokuwa na mwanzo hayana budi kuwa na mwisho. Dhambi yote haina budi kufikia maangamizi. Dhambi yote haina budi kuangamizwa kabisa. Kwa hiyo, katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu wakati ufufuo utakapokuja, haitatubidi kuzaliwa tena na baba zetu na mama zetu, lakini Mungu kama alivyofanya hapo mwanzo atamwita mtu kutoka katika mavumbi ya nchi, pamoja na msaidizi wake. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo alivyotenda jambo hilo hapo mwanzo.

⁹⁵ Kwa hiyo basi, Mungu habadilishi nia Yake kamwe juu ya jambo lo lote, bali atakuruhusu uendele. Sasa, hivi ni kupitia njia ya mzunguko sana kufikia yale ninayotaka kusema hapa juu ya jambo hili. Lakini, na, lakini, ni, uta-... nawatakeni mfahamu jambo hili. Mnaona? Mungu atakuruhusu kufanya jambo fulani, na hata akubariki katika kulifanya, bali hata hivyo si mapenzi Yake makamilifu.

⁹⁶ Mungu aliwaruhusu Israeli kuchukua amri, katika Kutoka sura ya 19. Wakati neema tayari ilikuwa imewapa nabii, Nguzo ya Moto, mwana-kondoo wa sadaka, nguvu za ukombozi, bali wao walililia wapate Amri. Haikuwa ni mapenzi ya Mungu, bali iliingizwa kwa kuwa mwanadamu aliitaka. Naye alilaaniwa na amri ile ile aliyotaka.

⁹⁷ Ni vizuri sana kuwa na mapenzi ya Mungu. Hivyo ndivyo alivyotufundisha. "Mapenzi Yako yatendeke. Ufalme Wako na uje. Mapenzi Yako yatendeke." Inatupasa kujikabidhi wenyewe kwenye mapenzi Yake na kwenye Neno Lake. Usilitilie swali. Liamini. Usijaribu kutafuta njia ya kuliepa. Lichukue tu jinsi lilivyo.

Watu wengi wanajaribu kuepa, kupitia njia nyingine. Nawe unapofanya jambo hilo, unajikuta ukipiga hatua, unakuta Mungu akikubariki, bali unafanya kazi katika mapenzi Yake ya kuruhusia wala si mapenzi Yake makamilifu, ya Kiungu.

⁹⁸ Yeye huliruhusu, kama nilivyosema, bali Yeye hata—Yeye hatalifanya liwe mapenzi Yake makamilifu; bali atalifanya litende kazi na kutukuza na kubariki mapenzi Yake makamilifu. Na kuzaa watoto, kwa kujuana kimwili, ni moja ya mambo hayo.

⁹⁹ Sasa angalia, Moabu, kwanza, lilikuwa taifa haramu. Lilianza, kiharamu, hata hivyo kwa ba—baba muumini na binti muumini.

Sawasawa tu, kama utafananisha jambo hilo na kutumia nia ya kiroho, unaweza kuona madhehebu hayo yamesimama pale dhahiri tu kama cho chote kile. Hakika. Mnaona, jambo hilo lote ni baya kwa jumla. Tena, angalia, linapoletwa, lilipoanza namna hiyo, haliwezi kamwe... Linaendelea, bongwe la theluji, linaendelea kuvingirika zaidi na zaidi na zaidi. Unapata kosa moja, na kuanza katika kosa hilo moja, nawe unaendelea tu kuviringisha jambo moja baada ya lingine, na jambo moja kama lingine, yote baada ya lingine.

¹⁰⁰ Na hivyo ndivyo kanisa lilivyoanza. Hivyo ndivyo lilivyoanza katika Nikea, Rumi, wakati Kanisa Katoliki la Kirumi... Hapo mwanzoni kabisa, mahali lilipotoka, palikuwa ni Pentekoste. Bali walipounda madhehebu na wakaingiza watu maarufu, kanisani, walianza kufanya, kuwa na maombi, na kuhesabu shanga, na—na kuwaombea wafu, na mambo hayo mengine yote. Halafu likaanza tu kuvingirika, kutoka kwenye kosa moja kuingia kwenye lingine, kosa moja kuingia kwenye lingine,

mpaka angalia mahali limeenda. Hakuna alama moja ya Pentekoste ndani yake, hata kidogo. Mnaona? Ni kosa moja likichukua lingine, likichukua lingine. Kuna jambo moja tu la kufanya, hilo ni, kufutilia mbali rekodi na kurudi kule mwanzo.

¹⁰¹ Wakati, Martin Luther alipoanza na kuhesabiwa haki. Hili linapaswa kuwa kanisa la Kiluteri, lililopiga hatua zaidi. Mnaona? Kama... Luther, wakati alipounda madhehebu, yeye hakuweza kuchukua utakaso wa Wesley, kwa maana alikuwa ameunda madhehebu; na watu hao wasingalivumilia jambo hilo, kwa hiyo Roho akatoka ndani yake.

¹⁰² Sasa, kundi la Lutu hapa; ama, Moabu alikuwa mtoto wa binti ya Lutu, wa haramu kwanza. Sasa angalia, kama kanisa la kawaida, Moabu, anawakilisha madhehebu ya kawaida.

Israeli inawakilisha Kanisa la kiroho. Israeli, kulikuwa na kanisa la kweli, lilikuwa ndilo bibi-arusi wa siku hizo, aliyeitwa kutoka Misri, na kuthibitishwa kuwa ni wa kweli.

¹⁰³ Angalia wakati wao, hao wawili walipokutana. Wote wawili walitoa sadaka ile ile, wote wawili walijenga, waliona madhabahu saba, wote wawili walitoa dhabihu safi, maksai. Nao hata walitoa kondoo dume, wakishuhudia ya kwamba Masihi yuaja. Kimsingi, wote wawili walikuwa sawa kabisa. Israeli, hapa chini bondeni; Moabu, huko juu kilimani. Nao Moabu wakiwa na madhabahu saba; Israeli na madhabahu saba. Moabu wakiwa na maksai saba; Israeli na maksai saba. Moabu wakiwa na kondoo dume saba, wakinena juu ya kuja kwa Masihi; Israeli wakiwa na kondoo dume saba.

Tofauti yao ilikuwa ni nini? Kimsingi, wote wawili walikuwa sahihi. Lakini, unaona, Moabu hawakuwa na thibitisho la Mungu miongoni mwao; wao walikuwa taifa tu, kundi la watu mashuhuri. Bali Israeli walikuwa pamoja na nabii. Walikuwa na Mwamba uliopigwa. Walikuwa na Nguzo ya Moto. Walikuwa na nyoka wa shaba, kwa ajili ya kuponya. Walikuwa na baraka za Mungu zikiambatana nao moja kwa moja, nao walikuwa watoto wa Mungu walioitwa watoke.

¹⁰⁴ Sasa tunaona jambo hilo limeonyeshwa hapa kikamilifu sana kwa mfano katika hayo makanisa ya siku hizi. Kwa vile, Moabu hawakuwa hivyo. Israeli walikuwa wasafiri, kutoka mahali pamoja kwenda mahali pengine; po pote Nguzo hiyo ya Moto ilipoenda, waliambatana Nayo. Moabu, sivyo; wao walikuwa wametulia kwenye madhehebu yao wenyewe, kule chini kwenye taifa lao wenyewe. Wao hawakusogea, walikaa huko huko. Wao walikuwa na watu wao mashuhuri. Waliamuru mambo jinsi walivyopaswa kufanya, nao walikuwa na mashujaa wao, walikuwa na askari wao wa vita, walikuwa na mfalme wao waliyekuwa naye, aliyewapa amri, na kadhalika.

¹⁰⁵ Lakini Moabu wakawaona Israeli wakiwa na kitu ambacho wao hawakuwa nacho. Waliona nguvu nyingi kati ya Israeli, na

zilikuwa nabii. Na nabii huyo alikuwa ni Musa. Nao walijua ya kwamba wakati vita vilipoenda mrama, wao waliinua tu mikono yake na kuishikilia juu kule, ndipo vita vikabadilika. Kwa hiyo hawakuwa na kitu kama hicho, kwa hiyo wao wanajaribu kukiambatanisha na siasa, na mvuto wa kisiasa. Waliagiza kwenye—kwenye nchi nyingine na kumwajiri nabii aje, kusudi waweze kuwa na nabii, nao wangukuwa na nguvu kati yao kama tu Israeli walivyokuwa nazo kati yao.

¹⁰⁶ Mnaona kujilinganisha kimwili? Mnaweza kuona kanisa la kimwili leo? Limefanya jambo lile lile.

¹⁰⁷ Angalia, sasa, wote wawili watakuwa na manabii. Tofauti pekee ilikuwa, Musa, nabii wa Mungu, Mfalme wake alikuwa ni Mungu. Huko ndiko alikotoa amri zake, Neno la Bwana. Naye Balaamu, yeye pia, yeye alikuwa na mfalme, na mfalme huyo alikuwa ni Balaki, mfalme wa Moabu, na huko ndiko alikotoa amri zake na baraka zake. Kwa hiyo Moabu akamwambia Balaki, “Shuka uje,” ama Balaamu, alisema, “shuka uje ukanilaanie watu hawa, kwa kuwa wanaufunika uso wote wa nchi. Wao wanakuja na kuramba kila kitu kama vile maksai anavyoiramba nyasi.” Kasema, “Shuka uje sasa. Nami nasikia ya kwamba unaweza kulaani, unaweza kubariki, kila ufanyacho kinatambuliwa.”

¹⁰⁸ Sasa, tunataka kuona ya kwamba mtu huyu alikuwa nabii aliyechaguliwa na Mungu, bali yeye aliuza haki zake za mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya sababu za kisiasa. Kama tu vile kanisa lilivyofanya leo, kama Luther, Wesley, Pentekoste, na kundi lote lao, wakaiuza yote kwa mivuto katika madhehebu yao. Musa, chini ya Mungu; Balaamu, chini ya Balaki. Hata hivyo, manabii wote wawili walikuwa watu walioitwa na Mungu, na wote wawili ni wa kiroho. Angalia tofauti. Kila mmoja alikuwa na kiongozi; wa Musa alikuwa ni Mungu; wa Balaamu alikuwa ni Balaki.

¹⁰⁹ Angalia hapa jinsi wa kiroho anavyotumiwa, kuthibitisha ya kwamba wa kawaida amekosea. Musa, aliyetumwa na Mungu, akiwa kazini, anakutwa na kusaiwa na nabii mwingine wa Mungu. Unaweza kuwazia jambo hilo! Musa, aliyetwa na Mungu, akachaguliwa na Mungu, amesimama kazini mwa Mungu; alisogea kwenye kundi hili baridi na la kawaida, naye akasaiwa na nabii mwingine wa Mungu, yule Mungu aliyekuwa amembariki na kumchagua. Ungejua je tofauti yake? Wote wawili walikuwa na manabii. Mungu alinena na manabii wote wawili.

¹¹⁰ Na baadhi yao husema, “Mungu alisema, ‘Fanya jambo *hili*.’ Mungu alisema, ‘Fanya jambo *lile*.’” Sasa, mimi silihoji hilo, bali haliambatani na Neno la Mungu. Nabii, haidhuru kama yeye ni nabii, yeye amekosea. Watu wengi sana hudanganywa namna

hiyo. “Loo, ndugu *huyu* anaweza kufanya jambo *hili*, na, ndugu *huyu* anaweza kufanya *lile*,” na kulikana Neno?

¹¹¹ “Nijaponena kwa lugha za wanadamu na za malaika, nijapokuwa na karama, kiasi cha kuhamisha milima, nijapotoa mali zangu zote kuwalisha maskini, ningali si kitu mimi.”

“Wengi watakuja Kwangu siku ile, na kusema, ‘Bwana, Bwana, sijatoa unabii katika Jina Lako? Hivi sijatoa, katika Jina Lako, hivi sijatoa pepo na kufanya kazi kubwa sana?’ Ndipo nitawaambia, ‘Ondokeni, enyi...Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Hata sikuwajua.’” Hata hivyo, walikuja na maungamo kwamba wamefanya jambo hilo, bali Yesu alisema, “Walikuwa watendao maovu.” Maovu ni nini? Ni jambo unalojua unapaswa kufanya, ambalo ni sahihi kufanya, na hata hivyo hulifanyi. Mnaona kitakachotukia katika siku za mwisho?

¹¹² Sikia jambo lote! Hilo ndilo lililokuwa kusudi langu usiku wa leo. Nilisema ningetoka kwenye saa tatu, lakini nitachelewa kidogo, labda. Angalia, hilo ndilo lililokuwa kusudi langu lote, kuwaonyesha jambo hili, kwa Neno la Mungu, mnaona, ya kwamba—ya kwamba Mungu hana budi kutimiza Neno Lake kusudi adumu kuwa Mungu.

¹¹³ Sasa, tunaona ya kwamba wote hawa wawili walikuwa watu wa kiroho, wote wawili walikuwa manabii, wote wawili walikuwa wameitwa. Naye Musa, akiwa moja kwa moja kazini, akiwa na Nguzo ya Moto mpya mbele yake kila siku, Roho wa Mungu akiwa juu yake, akiwa kazini. Huyu hapa mtumishi mwingine wa Mungu anakuja, aliyelitwa na Mungu, aliyechaguliwa na Mungu, nabii ambaye anajiliwa na Neno la Mungu. Hapa ndipo penye hatari. Hakuna mtu angaliweza kukataa mtu huyo kuwa ni wa Mungu—wa Mungu, kwa maana Biblia ilisema Roho wa Mungu alinena naye, naye alikuwa nabii. Lakini, unaona, alipopata jawabu halisi kutoka kwa Mungu, asingeitii. Hakuiona, ndipo akaenda kumsai Musa.

¹¹⁴ Sasa, Balaamu alitafuta mapenzi ya Mungu, kwa moyo wake wote. Sasa, wakati watu hawa mashuhuri walipokuja na kusema, “Balaamu! Mfalme Balaki ametumana, ya kwamba uje kwake mara moja ukawalaani watu hawa Israeli, kwa maana wao wamesambaa katika uso wote wa nchi, na sasa wao wamefanya kambi dhidi yangu. Nao wamepiga kila ufalme ulio karibu na hapa, chini yao. Basi sasa tunataka uje huku ukawalaani watu hawa. Kwa maana, nasikia ya kwamba ukimlaani mtu ye yote, amelaaniwa.” Sasa, unaona, yeye alikuwa mtu wa Mungu. “Unachobariki, kimebarikiwa.” Yeye alikuwa mtumishi wa Mungu.

¹¹⁵ Basi Balaamu sasa akawazia, akiwa nabii, “Kuna jambo moja tu kwangu kufanya, na hilo ni kutafuta kujua mapenzi ya Mungu ni nini.”

¹¹⁶ Hiyo ndiyo kazi ya nabii, kama ameitwa kuwa nabii. Kwanza, nabii anapaswa kufanya nini? Ni kutafuta kujua mapenzi, Neno la Mungu. Hana budi kufanya jambo hilo. Kwa sababu, akiwa nabii, Neno la Mungu linakuja kwake. Lile... Wao wanasema, “Vema, wewe si mwanatheolojia.” Kamwe Biblia haisemi ya kwamba Neno la Mungu humjilia mwanatheolojia. Wao ndio wanaolichafua. Neno humjia nabii wa Mungu.

¹¹⁷ Na hapa palikuwa na mtu ambaye alikuwa nabii wa Mungu. Na alipoajiriwa, kuajiriwa, aje na kuwalaani watu wengine wa Mungu, angalia, yeye aliondoka akaenda kutafuta kujua mapenzi ya Mungu. Naye alitaka kujua mapenzi Yake makamilifu, Naye Mungu akampa mapenzi Yake makamilifu katika jambo hilo. Yeye alipewa Mapenzi Yake makamilifu. Mapenzi Yake yalikuwa ni nini? “Usiende!” Hilo ndilo Neno la kwanza la Mungu. “Usiende pamoja nao. Usijaribu kuwashambulia watu Wangu, wanaotembea katika njia Zangu kamilifu.”

¹¹⁸ Jinsi jambo hilo lilivyo leo, wanataka kuzozana, kuhojiana, na cho chote kile, wanapona Roho wa Mungu akitenda kazi miongoni mwenu. Nao wanajaribu kuninii, wamejaribu jambo hilo kwa miaka mingi, kulisonga. Bali kadiri wanavyojaribu kulisonga, ndivyo linavyozidi kukua. Huwezi kulaani kile Mungu alichobariki. Huwezi kamwe. Huwezi kamwe kulifanya jambo hilo.

¹¹⁹ Kwa hiyo, unaona, hao walikuwa watu wa Mungu. Sasa, nabii huyo, ingawa alikuwa kule juu na aliajiriwa na mfalme, alifanya kazi miongoni mwa watu mashuhuri, na kadhalika. Nalo Neno la Mungu likamjia. Akatafuta kujua mapenzi ya Mungu, nayo mapenzi ya Mungu yakamjibu, yakasema, “Usiwalaani watu hawa! Niliwabariki.”

¹²⁰ Sasa hakuna mwanatheolojia chini ya mbingu anayeweza kukana Ujumbe huu tunaohubiri, ila kwamba ni Neno la Mungu katika wakati unaofaa kabisa. Mungu amekwisha uthibitisha, katika kila kitu ambacho kimesemwa ama kufanywa. Ameuthibitisha kuwa ni kweli. Sasa, hakuna mwanatheolojia, wala msomaji wa Biblia, wala nabii, anayeweza kuangalia katika Neno hilo, iwapo yeye ni nabii, ataona jambo lilo hilo. Bali kama yeye haoni jambo lile lile, hiyo inaonyesha kuna kasoro. Kwa maana...

¹²¹ Unasema, “Vema, loo, ningeweza kulichukua vingenevyo.” Vivyo hivyo, Balak, Balaamu waliweza. Mnaona? Bali Mungu alimtambulisha Musa.

Halafu thibitisho lilikuwa ni nini? Neno la Mungu. Naye alisikia maamuzi dhahiri na yaliyo wazi ya Mungu, “Usiende. Usijaribu ku—kulaani nilichobariki. Hao ni watu wangu.”

Bali unajua nini? Balaamu hakuwapenda watu hao, kwanza. Loo, ni... Kuna Balaamu wangapi ulimwenguni leo! Yeye hakulipenda kundi hilo, kwanza.

¹²² Sasa, baada ya yeye kupata maamuzi dhahiri ya Mungu, “Usiende.” Lakini, unaona, badala ya kufanya jambo hilo, lilikuwa ni jambo lile lile kama Kaini, kama Kora, yeye alikuwa na wivu, naye—naye alitaka ninii, sababu ya kwenda, kwa vyo vyote.

¹²³ Angalia, makao yake makuu ya kimadhehebu, baada ya yeye kurudi, yalisema, “La, sidhani nitashuka niende. Sidhani nitakuwa na uhusiano wo wote nao. Sitahojiana na hao watu, maana Mungu tayari amekwisha niambia wao ni watu Wake, nami siamini nitaenda.” Laiti angalidumu na jambo hilo!

Bali, ndani kabisa ya moyo wake, yeye hakuwapenda. Mnaona? Wao hawakuwa wa kundi lake. Na cho chote ambacho hakikuwa cha kundi lake, “hakikuwa sahihi, kwanza.” Mnaona? Naye akawadharau, kasema, “Kumekuwa na mambo fulani ya kuchukiza waliyofanya watu hao. Kweli Mungu mtakatifu atawalaani watu kama hao. Wao ni, wao hawajui kusoma. Hawana elimu kama sisi. Sisi ni watu werevu zaidi. Loo, wao wanadai kumtumikia Mungu, bali, waangalie, wao ni nini? Kundi la, mbona, kundi la watumwa, wakanyaga matope, ambao walifukuzwa na Wamisri kule chini. Naam, Mungu asingekuwa kamwe na uhusiano wo wote na kundi chafu kama hilo!”

¹²⁴ Alishindwa kuuona Mwamba ule uliopigwa na nyoka yule wa shaba, Nguzo ile ya Moto. Alijaribu kuwapambanua kimwili. Alishindwa kuona ule mwito mkuu zaidi wa Mungu. Kwa neema, kwa kuteuliwa, wao walikuwa kwenye mstari huo, na wakiwa na Neno la Mungu. Basi alipotaka kuwalaani, Mungu alisema, “Usifanye jambo hilo. Wao ni Wangu. Usiwasumbue. Usiwaguse.”

¹²⁵ Sasa, kwa hiyo mtu huyo akageuka, akarudi. Sasa angalia makao yake makuu ya kimadhehebu, hata hivyo, anaporudi. Wakatuma kundi lenye ushawishi mwingi zaidi. Wakati huu huenda kulikuwa na wengine, badala ya watu wa kawaida tu, huenda ni madaktari wa uungu waliokuja wakati huu. Huenda walikuwa maaskofu, ama labda wazee wa mikoa, kwa yote... Yeye alituma kundi bo—bo—bora, na kundi lenye ushawishi mwingi za—zaidi, mtu fulani aliyekuwa na elimu nyingi zaidi na angaliweza kuuelezea ule mpango vizuri zaidi, angeweza kuufanya uvutie.

¹²⁶ Unaona, hivyo ndivyo Kaini alivyofanya; alihoji. Hivyo ndivyo Kora alivyofanya; alihoji. Si yeye ahojiye.

“Tunatupilia mbali hoja.” Tunamwamini Mungu, haidhuru kitu kingine cho chote kinasema nini. Tunamwamini Mungu. Hatuhoji analosema Mungu. Huwezi kulihoji Hilo. Huna budi kulikubali kwa imani. Na cho chote unachojua, haikubidi kuhoji

tena. Sijui jinsi anavyofanya jambo hilo; ninaamini tu Yeye hulifanya. Sijui jinsi Yeye atakavyoitimiza ahadi hiyo; bali Yeye alisema angeitimiza. Ninaamini jambo hilo. Nalikubali kwa msingi kwamba ninaamini ni Neno la Mungu.

Unasema, “Vema, huwezi kujiepusha na jambo hilo.” Sijui jinsi nitakavyojiepusha nalo, bali Yeye alisema, “Liseme.”

Ninakumbuka mchungaji wangu wa Kibatisti aliniambia, kasema, “Mbona, Billy, utahubiria vizingiti kanisani. Mbona, unafikiri mtu ye yote atasikia kitu kama hicho?”

Nikasema, “Mungu amesema hivyo.”

“Utaweza je, ukiwa na elimu ya darasa la saba, kuwaombea wafalme, na kuhubiri kila mahali ulimwengu?”

¹²⁷ Nikasema, “Sijui nitakavyofanya jambo hilo, bali, Yeye alisema hivyo, na kwangu mimi hilo linatosha kabisa.” Mnaona? “Yeye alisema hivyo. Sijui jinsi litakavyotendeka.”

Akasema, “Unafikiri watu katika ulimwengu huu mkuu ulioelimika, ambao utapingana nao, juu ya somo hili la kuponya Kiungu na kadhalika, unafikiri wataamini jambo hilo?”

¹²⁸ Nikasema, “Si juu yangu kujua kama wao wataliamini ama hawataliamini.” Nikasema, “Wajibu wangu ni kulihubiri Hilo. Hivyo ndivyo alivyoniambia. Yeye alisema angekuwa pamoja nami, na akaniambia lingefanya nini.”

Na limefanya sawasawa kabisa kile Yeye aliishasema lingefanya: “Kwanza, shika mikono yao; baadaye itakuja kuwa ya kwamba hata utajua siri ya moyo wao.” Nami niliwaambia kuhusu jambo hilo, nalo limetimia hivyo. Linafanyaje jambo hilo? Ningali sijui jinsi linavyotendeka. Si kazi yangu jinsi linavyotendeka; linatendeka tu.

¹²⁹ Ni nani angeweza kueleza wakati Mungu alipomwambia Eliya, “Panda uende kule ukakae mlimani, nami nitakulisha. Nimewaamuru ku—kunguru wakulishe?” Kunguru angeweza kupata kipande cha mkate na kipande—kipande cha samaki, aliyekaangwa, na kumletea nabii? Hiyo ni zaidi ya kitu cho chote ningaliweza kuelezea. Wala sidhani hata wewe unaweza, ama mtu ye yote anaweza. Bali Yeye alifanya jambo hilo. Hayo tu ndiyo yaliyokuwa muhimu. Alifanya jambo hilo, na hiyo ndiyo kweli yake.

Jinsi alivyofanya jambo hilo, sijui; si kazi yangu. Bali alilifanya. Jinsi alivyoifanya dunia, sijui; bali aliifanya. Jinsi alivyomtuma Mwanawe, sijui; bali alimtuma. Jinsi alivyofufuka katika wafu, sijui; bali alifufuka. Aliniokoa namna gani? Sijui; bali aliniokoa. Hiyo ni kweli. Alikuokoa namna gani? Siwezi kukwambia; bali alikuokoa. Aliniponyaje? Sijui; bali aliniponya. Yeye aliahidi angefanya jambo hilo, Naye hulitimiza Neno Lake.

Sasa, Balaamu alipaswa kujua jambo hilo, naye alijua lililo bora zaidi.

¹³⁰ Angalia, kundi hili zuri, lenye ushawishi, lilikuja, na kitu gani kizuri zaidi? Walikuwa na zawadi nzuri zaidi. Isitoshe, wangeweza kumpa pesa nyingi zaidi, nao wangeninii— walimpa cheo bora zaidi. “Sasa, mbali na mhudumu wa kawaida tu katika madhehebu, tutakufanya mkuu wa wilaya. Mnaona? Kwamba, tuta—tutakufanyia jambo fulani kama tu utalifukuza kundi hilo la watu kutoka mahali pale, mnaona, na kukomesha jambo hilo.” Loo, wao walimpa cheo kikubwa. Kasema, “Kadiri unavyowabariki...” Kasema, “Wajua, mimi ninaweza kukupandisha cheo.” Angalia mahali anapotoa maneno yake, kiongozi wa nchi.

¹³¹ Musa alikuwa akitoa Maneno yake wapi? Mfalme wa Mbinguni. Mmoja alikuwa Neno la ahadi ya Mungu, “Nitawapeleka kwenye nchi ya ahadi, na hakuna mtu atakayesimama mbele zenu. Nitawatuma mavu mbele yenu na kuwafukuza, kutoka kushoto hata kulia. Nanyi mtaitwaa hiyo nchi. Nimewaa...Tayari nimewapa. Nendeni, itwaeni, mkaimiliki; ni yenu.” Na sasa, mnaona, Huyu ndiye Musa aliyekuwa anamsikiliza. Na mtu huyu alikuwa akisikiliza hata likafikia jambo moyoni mwake alilokuwa anaonea wivu, ndipo basi akamwendea mkuu wa dini yake. Mnaona?

¹³² Angalia, cheo kizuri zaidi. Akasema, “Unajua ninaweza kukupandisha cheo? Nitakupa cheo kizuri zaidi. Nitafanya mengi zaidi kwa ajili yako. Nitakuongeza mshahara. Nitakupa mshahara mzuri zaidi.” Basi alipompa haya yote, yalimpofusha.

¹³³ Ni Balaamu wangapi walioko ulimwenguni leo, ambao, kwa cheo kizuri zaidi, kanisa zuri zaidi, ahadi ya kitu fulani! Mtu anapofungua macho yake kwa Neno na kutenda kazi kwa Mungu... Na mtu huyo mzuri, ambaye ana ushawishi, ataanza kama mtumishi wa Mungu, naye anashikilia kusanyiko zuri. Baada ya kitambo kidogo, ubatizo wa Roho Mtakatifu unawekwa mbele yake; ubatizo katika Jina la Yesu unawekwa mbele yake, ambao ni Andiko na njia pekee ya Kimaandiko ya kubatiza. Na wakati huo unawekwa mbele yake, na hayo madhehebu yanajua yatampoteza akianza jambo hilo, wao wanampa cheo kizuri zaidi na badiliko kanisani. Mnaona, Ubalaamu wa kale, tena, sawasawa tu na ilivyokuwa hapo mwanzo.

¹³⁴ Sasa, mtu huyo anayesoma Biblia hiyo, hawezi kuisoma isipokuwa anaona kwamba jambo hilo ni Kweli. Hakuna mtu aliyewahi kubatiza akitumia vyeo vya “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Ni kanuni ya imani ya Katoliki wala si Fundisho la Biblia. Hakuna mtu katika Biblia aliyepata kubatizwa, ama miaka mia tatu baada ya kifo cha mtume wa mwisho, ila yule aliyebatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Kanisa Katoliki lilianzisha jambo hilo, na hayo mengine yakaliendea. Na mhudumu ye yote anayeketi kwenye chumba chake cha kusomea na ataangalia jambo hilo, anajua ya kwamba jambo hilo ni

Kweli. Lakini, kwa kupendwa na watu wengi, kushikilia mahali pake, kuwaziwa mema kati ya watu, yeye anapatana.

“Vema,” unasema, “Mungu alimbariki.”

¹³⁵ Bila shaka. Wengine wao wana karama za kuponya; wengine wao wana mikutano mikubwa. Na jambo hilo limesuguliwa moja kwa moja usoni mwao, nao wanapata jawabu ile ile kutoka kwenye Neno la Mungu ambalo wewe ama mtu mwingine ye yote angepata. Mungu habadiliki. Mnaona ninalomaanisha?

¹³⁶ Balaamu, kwa ajili ya cheo kizuri zaidi, alifikiri. Sasa angalieni, wakati kundi hilo bora zaidi liliporudi, ninii halisi. . . Balaamu, hapa, alichukua fungu bandia la maneno. Mnaona? Yeye alisema. . . Ku—kundi lililo bora zaidi likarudi, a—alipaswa kusema, “Ondokeni mbele zangu! Nimewaambia Neno la Mungu. Nendeni zenu! Hii ni BWANA ASEMA HIVI.” Lakini, mnaona, zile zawadi, na kuwa mtu anayependwa zaidi na watu!

¹³⁷ Loo, jinsi wanavyopenda kufanya jambo hilo. “Tutakutuma kila mahali ulimwenguni. Tutakupua ndege maalum. Tutadhamini mikutano yako kila mahali kama utaninii tu. . .” Loo, la. A-ha. Mnaona?

Tunajua vile Neno lisemavyo. Tunajua alichosema Mungu. Tutadumu na hicho, kwa msaada wa Mungu. Mnaona? Haidhuru ni ahadi ya namna gani, na unaweza kulipa kiasi gani zaidi, na ni ngapi *hii*, *ile*, ama *nyingineyo* unaweza—unaweza kutoa; tunataka BWANA ASEMA HIVI, na lile alilosema *Hapa* kwanza.

“Vema, kanisa lilisema, ‘Hilo si muhimu.’”

Tunataka lile alilosema Mungu hapo mwanzo. “Na lo lote likiongezwa ndani Yake ama kutolewa Kwake, hata jina lako litaondolewa kwenye Kitabu cha Uzima; kuongeza neno moja Kwake, ama kutoa Neno moja Kwake.” Tunataka alichosema Yeye; si kile kanisa lilisema, kile alichosema Daktari Jones, kile alichosema mtu mwingine. Tunataka kile BWANA ASEMA HIVI ilichosema, kile Neno lilichosema.

¹³⁸ Bali sasa tunaona Balaamu, mtumishi wa Mungu. Na wengi wa hao watu huanza, nao wamechaguliwa na Mungu, nao kweli wananena Neno la Mungu katika mambo mengi; bali inapofikia kwenye ile Kweli kamilifu, wao hawatafanya jambo hilo.

¹³⁹ Angalia hapa, kama nabii wa Mungu, haikumpasa kukutwa kwenye kundi kama hilo, kwanza. Haikumpasa kwenda pamoja nao. Bali, angalia, kwa ajili ya kupendwa na watu, mnaona, kwa ajili ya dhamira yake, alisema, “Vema, kaeni usiku kucha, nami nitajaribu tena.” Mnaona, “Nitajaribu tena”? Unataka kujaribu tena kwa nini?

¹⁴⁰ Mungu tayari amemwambia la kusema. Mungu alisema, “Waambie huendi.” Hilo ndilo Neno Lake la awali. “Mimi siendi. ‘Nawe usiende. Usilaani nilichobariki.’” Sasa angalia,

jambo hilo lilimrudia, baada ya kitambo kidogo. Mnaona? Na litafanya hivyo, kila wakati. Mungu anaposema jambo lo lote, anamaanisha jambo hilo. Yeye habadilishi nia yake juu ya jambo hilo. Anakaa moja kwa moja na Neno Lake. Haidhuru mtu mwingine ye yote anasema nini, Yeye anakaa moja kwa moja na Neno hilo.

¹⁴¹ Sasa, Balaamu alipaswa kujua vema zaidi. Alipaswa kujiondoa kutoka katika kundi kama hilo, bali hizo zawadi zote nzuri na a—a—ahadi ambayo mfalme huyu alisema, “Unajua naweza kufanya jambo hilo. Mimi ndimi askofu. Ninaweza kufanya cho chote nitakacho tu, nami nitakupandisha cheo kama utakuja na kunifanyia jambo hilo.”

Na Mungu tayari alikwisha kumwambia, “Usifanye jambo hilo,”

¹⁴² Bali hata hivyo Balaamu alisema, “Wewe, wewe kaa usiku kucha, nami nita—nitajaribu tena.”

Mnaona, yeye alikuwa na Neno. Haikubidi kubishana tena juu ya jambo Hilo. Mungu tayari amekwisha kusema jambo hilo. Ukiwa na kundi kama hilo, daima watakushawishi toke katika mapenzi ya Mungu, kama ukiwaruhusu.

¹⁴³ Kulikuwa na kundi moja lililomjia nabii, wakati mmoja, aliyeitwa Ayubu. Wasingeweza kumshawishi. Yeye aliona ono. Alijua lililokuwa sahihi.

Balaamu aliona ono, na hata hivyo hakukaa Nalo.

¹⁴⁴ Haidhuru makundi yake ya kanisa yalisema mengi jinsi gani, “Loo, Ayubu, unapaswa kufanya jambo *hili*, unapaswa kufanya jambo *lile*.” Hata mkewe, alisema, “Unazungumza kama mtu mpumbavu.” Mnaona? “Ninajua yale aliyosema Bwana. Ninajua kile alichohitaji, na hicho ndicho nimefanya.” Mnaona, yeye alidumu na kile Mungu alichomwambia.

¹⁴⁵ Angalia, Balaamu akitumia kifungu hiki cha bandia kwa ajili ya dhamira yake. Mnaona? Alisema, “Vema, “Nita—nitatafuta kujua. Nitajaribu tena.” Sasa, hapo ndipo unapokuja, mara ya pili. Ni Balaamu wangapi tulio nao usiku wa leo, wanaopenda kutumia kifungu hicho bandia cha Mathayo 28:19 [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbara mara tatu—Mh.] kwa ajili tu ya dhamira zao? Ni wangapi wanataka kutumia Malaki 4 kwa ajili ya dhamira zao? Ni wangapi wanataka kutumia Luka 17:30 kwa ajili tu ya dhamira zao? Ni wangapi wanataka kutumia mambo haya, hata hivyo, “Vema, nawaambia, ni—ninaamini wao wamechanganyikiwa kabisa juu ya jambo Hilo?”

¹⁴⁶ Halafu hapa alikuwepo Balaamu akijaribu kusema, “Labda huenda ikawa Mungu alichanganyikiwa. Nitajaribu tena, mnaona, nione alilosema.” Sasa, Yeye anajua moyo wako. Angalia, Balaamu alitumia fungu hili la bandia kwa ajili ya

dhamira yake, kwa maana, kweli, alitaka fedha hizo. Alitaka umashuhuri huo. Alitaka hiyo. Alitaka kazi hiyo. Alitaka cheo hicho, kuangaliwa, kama Daktari *Fulani*. Kwa hiyo a— a—akasema, “Nitajaribu tena.”

147 Loo, akina Balaamu ulimwenguni usiku wa leo, walioahidiwa vyeo, kupendwa na watu! Jamani, loo, jamani! Wanatia ganzi dhamira zao kwa vitu hivyo. Kwa sababu ya madhehebu yao, wao wanasema, “Kama ukifanya jambo *hilo*, utaondolewa. Najua wewe ni mtu mzuri, nasi tunakupenda,” naye ni mtu mzuri, “tunakupenda. Bali huwezi kuhubiri hayo. Ma—mafundisho yetu yanasema huwezi kufanya hivyo. Daktari *Fulani* alisema hivi ndivyo ilivyo. Sasa huna budi kuamini namna hii, kama ukikaa pamoja nasi. Sasa, ukitaka kufanya hivyo, najua ulikuwa na wakati mgumu, vema, nitaona kama siwezi kukufanya upandishwe cheo, labda ubadilishe makanisa.” Loo, ewe Balaamu! Ukijua mapenzi ya Mungu, yatekeleze! Mungu hatabadilisha nia Yake. La.

148 Kitu ambacho Yeye angekipuza, ile kweli, kwa ajili ya agizo lake. Alisema, “Vema, Nita—nitajaribu tena.” Angalia akina Balaamu waliopo.

149 Kwa hiyo sasa kumbuka, alipokuja usiku wa pili, pamoja na watu hawa mashuhuri sana, tayari dhamira yake ilikuwa nzito na yenye ganzi, Mungu akamruhusu aende. Sasa, Mungu kamwe hakubadilisha nia Yake, bali alimpa mapenzi Yake ya kuruhusia. “Haya nenda basi.” Bali alitambua haitafaulu.

150 Mungu alijua kilichokuwa katika moyo wa Balaamu. Ingawa alikuwa nabii, alijua aliwachukia hao watakatifu wanaojifingirisha, naye—naye alininii tu...ali—alikuwa anataka kuwalaani, kwa vyo vyote. Naye Mungu tayari alikuwa amemwambia asifanye hivyo, bali hata hivyo akaja, alitaka kufanya jambo hilo, tena, kwa hiyo Mungu akamwacha aende zake. Mungu akasema, “Haya nenda.” Basi, kumbukeni, Yeye hakubadilisha nia Yake kamwe.

151 Angalia, shauku yake ilikuwa ni kuwalaani. Watu aliowaona kama washupavu wa dini, alitaka kuwalaani. Alitaka cheo. Hakutaka kucheza nao, kwa hiyo alifikiri kama angeweza kufanya tendo hili dogo kwa ajili ya mfalme, basi angepandishwa cheo. Mungu kamwe hakubadilisha nia yake wala Neno Lake.

Bali atakupa mapenzi ya moyo wake, ya moyo wako. Yeye aliahidi jambo hilo. Unajua hivyo? Aliahidi kukupa shauku ya moyo wako. Basi hebu shauku yako iwe Neno la Mungu. Hebu shauku yako iwe ni mapenzi Yake, si mapenzi yako mwenyewe. Mapenzi Yake! Kama Yeye...Ukimwomba Yeye kitu fulani, asikupe, sema, “Asante, Bwana. Unajua kinachofaa.”

¹⁵² Angalia hata Mfalme Hezekia, wakati alipomtuma nabii yule kule kwake, Mungu alifanya hivyo, kisha akasema, “Tengeneza mambo ya nyumba yako. Utakufa.”

Hezekia alielekeza kichwa chake ukutani akalia kwa uchungu, na kusema, “Bwana Mungu, na—nakuomba unifikirie. Nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu. Nakutaka uniruhusu kuishi miaka kumi na mitano zaidi.”

¹⁵³ “Vema.” Mungu akanena na nabii, akasema, “Nenda ukamwambie nilimsikia.”

Basi alifanya nini? Alileta aibu kwa taifa zima. Aliichochea gadhabu ya Mungu hata angalimwua. Hiyo ni kweli. Mnajua jambo hilo. Akarudi nyuma akamwacha Mungu. Ingalikuwa vema sana, zaidi, kwa taifa, mfalme, na wote, kama angalienda zake na kuchukua jambo la kwanza la Mungu kwake.

Bali lilionekana jambo gumu kwa nabii, wakati ilimbidi nabii kurudi na kunena Neno la Mungu kwake, baada ya kumwambia. Lakini Mungu alisema, “Haya nenda.” Lakini, mnaona, jambo hilo lilileta aibu.

¹⁵⁴ Balaamu alifanya nini? Baada ya kujua mapenzi ya Mungu, na hata hivyo alikuwa anashikilia, alikuwa atafanya jambo hilo, kwa vyo vyote. Basi lilifanya nini? Angalia. Yeye kamwe hakubadilisha nia Yake. Yeye alijua kilichokuwa moyoni mwake.

¹⁵⁵ Mwajua, Tomaso, wakati mmoja yeye hakuweza kuamini. La, a—alisema, “Sasa, siwezi kuamini hilo. Kama ningaliweza kuchukua mkono wangu na kuuweka ubavuni Mwake, niuweke kwenye misumari ya mkono Wake, vema, basi, basi nita—nitaamini basi.”

Akasema, “Njoo hapa, Tomaso. Mnaona? Sasa ingiza mikono yako hapa ndani.”

Sasa, loo, Tomaso akasema sasa, “Ni Bwana wangu na Mungu wangu.”

¹⁵⁶ Kasema, “Naam, umeona, na sasa unaamini. Ni zaidi sana vipi thawabu yao, wasiopata kuona na hata hivyo wanaamini!”

Watu wakati mwingine hawatampokea Roho Mtakatifu isipokuwa wanene kwa lugha. Ninaamini katika kunena kwa lugha, bila shaka. Yeye ni Mungu mzuri; atakupi shauku ya moyo wako. Bali haidhuru unanena kwa lugha kiasi gani, na kulikana Neno hili, umekosea hata hivyo. Mnaona? Manaona, huingii kwa kunena kwa lugha. Unaingia kwa kutimiza kila Neno. Huo ndio ushuhuda wa kuwa na Roho Mtakatifu, unapoamini Neno la Mungu. Mnaona?

¹⁵⁷ Ninaamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini unaweza kuhuishwa, kama nilivyosema asubuhi ya leo, hata unene kwa lugha mpya. Nimefanya hivyo, mimi mwenyewe, nami ninajua ya kwamba ni Kweli. Najua ni kweli. Bali hiyo siyo ishara, wewe,

ya kwamba wewe ni mtoto wa Mungu aliye chaguliwa. Mnaona? La, hashu. Yeye hakusema kamwe. . .

“Wengi watanijia na kusema, ‘Bwana, sijatabiri na kufanya mambo haya yote makuu katika Jina Lako?’ Yeye atasema, ‘Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu, sikuwajua Mimi.’”

¹⁵⁸ Unanena kwa lugha kisha unakataa kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo? Kuna kasoro mahali fulani. Naam, bila shaka; mojawapo ya mambo hayo, mojawapo ya maagizo hayo aliyotoa Mungu. Kuna kasoro. Chunguza tu dhamira yako mwenyewe, na uone vile—uone vile ilivyosema Biblia. Nionyeshe mahali fulani ambapo mtu fulani alibatizwa katika Jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Mnaona? Hakuna. Lakini, mnaona, wakati mwingine kwa ajili ya dhamira yako, unasema, “Vema. . .”

Unasema, “Mungu hunena na wanawake juu ya kile wanachopaswa kufanya, si kuvaa kaptura na kadhalika, lakini, wajua, mchungaji alisema. . .” Kwa hiyo wao wanachukua njia iliyo rahisi.

¹⁵⁹ Wanajua kile Mungu alichosema juu yake Hapa. Mnaona? Hakika, Mungu alisema hivyo.

Kwa hiyo wao—wao—wao wanataka kufanya jambo hilo, kwa vyo vyote, mnaona. Wanajaribu kupata udhuru. “Vema, nafikiri ni bora zaidi. Ni—si. . . Upepo hauvumi. . .” Naam.

Bali Mungu alisema mwanamume avae tofauti na mwanamke. “Kama mwanamke akivaa vazi lililompasa mwanamume, ilikuwa ni chukizo mbele Zake.” Kwa hiyo si sahihi, ndiyo, nawe hupaswi kufanya jambo hilo. La. Mnaona? Kwa hiyo, basi, ni kosa.

¹⁶⁰ Lakini, unaona, wao wanajaribu kupata udhuru, kwamba, “Bwana aliniambia nifanye jambo hili.” Sisemi Yeye hakukwambia hilo, lakini, angalia, si mapenzi Yake makamilifu. Hapana budi ni mapenzi Yake ya kuruhusia. Unaona yatakavyofanya? Yataharibu kundi lote. Yaliharibu kambi yote.

¹⁶¹ Angalia hapa, Mungu hakubadilisha nia Yake kamwe, Neno Lake. Bali Yeye ni Mungu mwema, Naye atakupa shauku ya moyo wako, ingawa itakuwa ni kinyume cha mapenzi Yake. Mnaamini jambo hilo?

Tazameni, Mungu alimwambia Musa, “Shuka uende kule,” nabii huyu aliyetiwa mafuta. Kasema, “Shuka uende kule ukauambie ule mwamba.” Umepigwa tayari.

¹⁶² Musa akashuka akaenda kule katika hasira yake, akaitwaa fimbo, akasema, “Enyi waasi, ni lazima tuwatokezee maji katika mwamba huu?” kisha akaupiga ule mwamba tena. Maji hayakutoka. Akaupiga tena; yakatoka. Jambo hilo lilikuwa dhidi ya mapenzi ya Mungu. Lilivunja kila mpango katika Biblia; Kristo alipaswa kupigwa mara ya pili. Mnaona?

Kristo alipigwa mara moja. Lilivunja mpango wote. Bali Yeye alimpa mapenzi Yake ya kuruhusia. Kisha, baadaye, akasema, “Mnaona, tuna maji kwa ajili yenu. Naam, nimeyaleta kwa ajili yenu, enyi kundi la waasi!”

¹⁶³ Mungu akasema, “Njoo huku, Musa. Njoo huku. Njoo huku juu. . . Umekuwa mtumishi mwaminifu.” Kama yule mwanamke mwenye viatu vyenye visigino virefu, “Ulipanda, unaona. Angalia kule ng’ambo. Unaona ile nchi ya ahadi?”

“Ee, Bwana!”

“Lakini wewe hutaenda kule. Ulichukua mapenzi Yangu ya kuruhusia, huku chini kwenye Mwamba. Umejitukuza, unaona, wala si Mimi. Ulijitakasa. Hukunitakasa Mimi. Hukutimiza Neno Langu la asili, nilichokwambia ufanye.” Hata hivyo maji yalikuja kweli.

Unaweza kuweka mikono yako juu ya wagonjwa nao watapata afya. Unaweza kutoa unabii, ama kunena kwa lugha. Bali, jambo ni kwamba, timiza Neno Lake la asili! Mungu habadilishi nia Yake, ewe rafiki. Huna budi kutimiza agizo Lake, mapenzi Yake.

“Loo, vema, hilo lilikuwa kwa ajili ya wale wanafunzi!”

¹⁶⁴ Yeye habadiliki. Kama angali ana mwanafunzi, hilo ni agizo lile lile. “Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Haijabadilika. Yeye hawezi kubadilika.

Sasa, unaweza kusema, “Vema, nakwambia, si kwa ajili ya siku hizi.” Loo, Balaamu wee! Unaona? Unaona, Mungu habadiliki. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁶⁵ Hebu waangalie tu akina Balaamu leo. “Loo, najua, katika Biblia wao walibatiza katika Jina la Yesu, lakini, angalia, watu wote. . .”

Sijali watu wamefanya nini. “Hakuna Jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu ambalo unaweza kuokolewa kwalo.” “Hakuna msamaha wa dhambi, ni katika Jina la Yesu Kristo tu.” Jinsi, jinsi ulivyo mwema, unachofanya, hilo halina uhusiano wo wote nalo. Ni Neno la Mungu la asili; huna budi kudumu na hilo. Whiu! Vema.

¹⁶⁶ “Utii wa Neno Lake ni bora kuliko dhabihu.” Mnakumbuka ule wakati Sauli aliporudi.

¹⁶⁷ Balaamu alikuwa na karama ya imani na angaliweza kuitumia kwenye Neno la Mungu lililo kamilifu na la asili.

Watu wengi kwenye huduma leo, wenye karama za uponyaji, wangeweza kufanya jambo lile lile. Watu wengi huku nje, watu wanaonena kwa lugha, watu wanaotoa unabii, karama, wangeweza kuitumia kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, bali wao hawafanyi hivyo. Wao wanachukua. . . Na Mungu huwabariki,

hata hivyo, wanapata mapenzi Yake ya kuruhusia. Bali kwa ajili ya kupendwa na watu wengi, na anasa, faida za kibinafsi, waliuza haki zao za wazaliwa wa kwanza, kama alivyofanya Esau, mnaona, wakajiuza kwa madhehebu. Wakajiuza, kama alivyofanya Balaamu. Mnaona?

Wengi sana wanafanya leo jambo lile lile. Tunajua jambo hilo ni kweli. Wanauza haki yao ya mzaliwa wa kwanza. A-ha! Wanawake wanaomkiri Roho Mtakatifu, wakivaa kaptura; wanaume wakiwaruhusu mimbarani, wanawake waliokata nywele zao mimbarani; vipodozi usoni mwao, wamevalia majoho ya kidini. Jiwe kuu sana la kujikwaa kanisa liliwahi kuwa nalo.

¹⁶⁸ Ukitaka kujua, katika nguvu za kisiasa, ni saa ngapi katika majira ya Ufalme, angalia mahali walipo Wayahudi. Angalia jinsi Wayahudi walivyo, kwa maana wao ni taifa. Ukitaka kujua mahali mataifa yanasimama, waangalie Wayahudi.

Ukitaka kujua mahali kanisa limesimama, waangalie wanawake. Angalia uadilifu miongoni mwa wanawake, maana yeye ni mfano wa kanisa. Unapooni upotovu miongoni mwa wanawake, utaona mchafuko kanisani. Anachokuwa, Yezebeli aliyejipodoa, ndivyo hasa kanisa limekuwa. Mnaona? Sasa, hiyo ni kweli, nawe unajua jambo hilo. Uaona? Ukitaka kujua mahali lilipo kanisa, angalia uadilifu miongoni mwa wanawake wenu. Maana, yeye ni, kanisa ni mwanamke.

Ukitaka kujua hali za kimataifa, waangalie Wayahudi.

¹⁶⁹ Angalia, kama Mungu alivyomwambia Balaamu, baada ya kusikia uamuzi wa kweli wa Neno, "Usiende." Naam, kisha akamwambia, baada ya Yeye kuona jambo hilo moyoni mwa—mwake, alilipaswa kufanya; Yeye alimpa mapenzi Yake ya kuruhusia, kwa hiyo akasema, "Nenda."

¹⁷⁰ Nawe unaweza kufanya jambo lile lile. Kama hutaki kutembea katika Kweli, unaweza kuondoka uende na uwe—uwe na huduma kubwa. Bila shaka, unaweza. Bali unachukua mapenzi Yake ya kuruhusia. Unakanyaga-kanyaga Neno Lake. Yeye atakufanikisha, bila shaka. Ile. . .

Kama vile tu alivyomfanya Balaamu. Yeye alifanikiwa, bali asingaliweza kuwalaani wale watu. Asingeweza kuwalaani. Maana, kila alipoanza kulaani, alibariki. Mnaona, asingeweza kuwalaani. Bali ilipofikia kufanikiwa katika ufanisi wake, aliwafundisha watu wale, kupitia kwa Balaki, kufanya uzinzi. Aliwaleta kwenye kambi ya Israeli na kuwaoza, kasema, "Mbona, sisi sote ni mmoja. Mbona, ninyi mmemwabudu Mungu yule yule. Tuna nabii hapa; nanyi mna nabii kule chini. Nasi tuna dhabihu ile ile, Yehova yule yule kama baba zetu. Sasa, mbona ninyi nyote msije mkashirikiane nasi."

Biblia ilisema, "Msijiunge na wasioamini, msijifunge nira pamoja nao, hata kidogo. Iwapo hawaliamini Hilo, msiwakaribie." Mnaona? "Tokeni, mkatengwe," asema Bwana,

“Nami nitawapokea.” Mnaona? “Msiguse vitu vyao vilivyo vichafu.” Hiyo ni kweli. Uchafu wao dhidi ya Neno, na vitu kama hivyo, msiukaribie. Msiusikilize.

¹⁷¹ Na hapa tunapata kwamba Balaamu alishuka akaenda kule naye akaanza kuwafundisha hao watu, naye alikuwa na kosa. Naye—yeye aliifuata njia ya Balaamu, jinsi alivyofanya, na kumfundisha Balaki, na wana wa Israeli wakafanya uzinzi. Ndipo tauni ikalipiga taifa la Israeli, hao watu, na maelfu yao wakafa katika siku moja.

Basi wote walipokuwa pale, mbele ya madhabahu ya Mungu, wakiomba, huyu hapa mwanamume Mwisraeli pamoja na mwanamke Mmidiani, mwanamke wa kimadhehebu, wakaingia hemani. Ndipo mwana wa kuhani akaenda kule, akachukua fumo na kuwaua wote wawili. Basi jambo hilo likazuia ghadhabu ya Mungu. Mnajua hayo ni Maandiko. Sivyo? Mnaona?

¹⁷² Bali nini kilitukia? Balaamu, alifaulu katika kuwadhoofisha Israeli. Alifanya nini? Alidhoofisha kambi yao. Mungu alimwacha aondoke aende akaidhoofishe kambi yao, na jambo hilo likaharibu kambi yote.

Na wakati mafundisho fulani yanapoanza, ambayo si Kweli ya Biblia, yanaharibu kambi nzima. Mtu fulani anainuka akiwa na wazo tofauti, kama Kora, na kusema, “Vema, *hili, lile*, na *lingine*, nami nina wazo tofauti,” linachafua kambi yote. Na hivyo ndivyo limefanya kambi yote ya kanisa leo. Hiyo ni kweli.

¹⁷³ Kufundisha kama alivyofanya, akidhoofisha kambi yote kwa ajili ya Kadeshi-Barnea, shindano la kuamua la Neno. Walipofika Kadeshi-Barnea, basi, kule kuidhoofisha kambi. Wakarudi. Walikuwa wamefuata moja kwa moja. . .

Kumbukeni, wao walikuwa wamekula chakula cha Malaika. Wao walikuwa na Neno la Mungu, kila usiku, lililodhihirishwa. Nao wakala hicho chakula. Wakaunywea ule mwamba. Walifanya yote, waliona ile miujiza. Walimwalia Musa, na kuona neno lake, wakaona unabii wake, kila kitu.

Ndipo hatimaye wakati walipomsikiliza mwalimu huyu wa uongo, aliyekuja miongoni mwao na kufundisha makosa, akaidhoofisha kambi, na kufanikiwa kwa jambo hilo.

Huenda alijenga mijengo ya dola milioni moja. Huenda alikuwa na madhehebu makubwa. Huenda aliongezea maelfu mara elfu nyingi, na kufanya kazi kubwa, na kazi kuu, na alikuwa nabii. Hiyo ni sawa, bali, mradi tu haiambatani na Neno la Mungu, afadhali usiikaribie.

Mungu habadili nia Yake. Kaa moja kwa moja na Neno Lake, maana hilo ndilo litakalotokea mwishoni, lile Neno, Neno kwa Neno. “Ye yote atakayeondoa Neno moja Kwake, ama kuongeza neno moja Kwake!” Halina budi kudumu, Neno hilo.

¹⁷⁴ Sasa sikilizeni kwa makini basi. Wakati jaribio la Neno lilipokuja, walipovuka na kuona upinzani ukiwa mkubwa sana, upizani mkubwa sana waliopata kuona, Waamaleki walikuwa—walikuwa mara kumi ya ukubwa wao. Wakasema, “Tunaonekana kama panzi. Kuta zao, ama miji yao imezungushiwa kuta sana hata wanaweza kufanya mbio za magari kuzizunguka, magari mawili, wakiendesha kasi sana wawezavyo kwenda, kuzizunguka hizo kuta, mnaona, za miji yao. Mbona, mikuki yao imefikia kule mbali, ni mirefu. Nao ni majitu. Mbona, tunaonekana kama panzi. Hatuwezi kufanya jambo hilo.”

Ndipo watu wawili wakasimama kwenye hilo Neno, Kalebu na Yoshua, wakasema, “Ngojeni kidogo! Enyi watu milioni mbili nyamazenini kidogo tu. Sisi tunaweza kabisa kufanya jambo hilo na zaidi. Mnaona, sisi tu tunaweza kuwashinda bila shaka.”

Wao walikuwa wakiweka hilo juu ya msingi gani? Mungu alisema, “Nimewapa hiyo nchi. Ni yenu.” Nao hao hapo wamesimama. Bali watu walikuwa wameoana, miongoni mwa mambo mengine, na kila namna ya kanuni za imani na desturi kati yao, nao wamedhoofika tu, hafifu, hawakujua wageukie njia gani wala wafanye nini. Hiyo ni kweli. Jaribio la Neno likaja.

¹⁷⁵ Hata hivyo, Yeye hukupa ruhusa kufanya, huruhusu shauku yako, mapenzi ya kuruhusia, akijua ya kwamba. . . Kile kilicho ndani ya moyo wako, Yeye anakijua.

Unasema, “Vema, Ndugu Branham, mimi hufanya *kadha* na *kadha*. Halinisumbui. Mungu hunibariki kila siku. Mimi huimba katika Roho. Mimi hucheza katika Roho. Mimi. . .” Yeye ataruhusu jambo hilo. Endelea. Hiyo ni kweli. Bali utafanya nini?

¹⁷⁶ “Mimi huvaa kaptura, nami hufanya jambo *hili*. Halinisumbui. Najua imani yangu imo katika Kristo, si katika kile ninachovaa.”

Lakini, Biblia ilisema kuna kitu, pia. Unaona? Utafanya nini? Utafanya jiwe la kujikwaa, kama Balaamu alivyofanya, mbele ya kila mmoja wa hao wanawake wengine. Utafanyaje kwa wasichana wako wadogo? Utakuwa na kundi la akina Ricketta, hiyo ni kweli kabisa, kundi la Mayezebeli wadogo waliojipodaa. Unaona?

¹⁷⁷ Bali Mungu atakufanikisha. “Mbona, Yeye hunibariki.” Sitilii shaka jambo hilo. Alimbariki Balaamu, pia. Unaona? Bila shaka atakubariki. Utatembea katika mapenzi Yake ya kuruhusia, sio mapenzi Yake makamilifu. Mungu habadilishi nia Yake, maana anakubariki.

Yeye aliwabariki Israeli kule nje kwa miaka arobaini. Wao walifanya nini? Walioa wake, wakalea jamaa, wakawabusu watoto, wakalipa zaka zao, wakaishi moja kwa moja kule nje. Naye Mungu aliwabariki jangwani, akawalisha mana, siku

baada ya siku. Na kila mmoja wao aliangamia, kwa maana wao hawakutimiza mapenzi Yake ya awali, ya kuruhusia... Mapenzi Yake ya awali, Neno Lake. Walichukua mapenzi Yake ya kuruhusia.

¹⁷⁸ Endeeleni, bali, kumbukeni, walipoondoka Kadeshi, wao hawakusafiri mbele zaidi. Walizunguka tu na kuzunguka, jangwani. Wakati, wao wangaliweza kutoka, katika siku mbili baadaye, wangaliweza kuwa katika nchi ya ahadi. Walisafiri kwa muda wa miaka arobaini, na kila mmoja wao akafa ila Yoshua na Kalebu, hao waliodumu katika Neno la asili.

¹⁷⁹ Ee Mungu, tusaidie. Mungu habadilishi mapenzi Yake. Yeye habadilishi nia Yake, bali atakubariki.

Hakika, Yeye alimbariki Balaamu. Naye alifanyaje kule chini? Alichafua kambi yote. Mnaona, inakubidi kudumu na kile alichosema. Yeye hakubadilisha kamwe mpango Wake wa asili.

¹⁸⁰ Sasa waangalie akina Balaamu leo, hudumani, waangalieni. Angalieni tu kila mahali. Wakifanikiwa, wakinena kwa lugha, hakika, wakitumia karama ya Mungu wapate faida, kila kitu, hakika. Bali jambo hilo linalichafua kanisa lote la Mungu kwa mafundisho yao yaliyopotoka. Hiyo ni kweli.

Mtu mmoja aliniambia, akasema, “Mbona unafanya jambo *hili*? Mbona unafanya jambo *hilo*?”

Nikasema, “Hivi huamini ya kwamba hilo ni Kweli?”

¹⁸¹ “Loo, naam. Lakini,” akasema, “unajua nini? Hiyo si kazi yako. Unapaswa kuwaombea wagonjwa. Wao wanaamini kwamba wewe ni nabii. Mbona, ungewafundisha hao wanawake jinsi ya, na hao wanaume, jinsi ya kufanya jambo *hili*, *lile*, na *linginelo*.”

“Ungewezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatajifunza ABC? A-haa? A-haa? Ungewezaje kuwafundisha mambo wakati hata hawatachukua kitabu cha masomo ya kwanza?” Unaona? Huna budi kurudi na kuanzia mahali ulipoanzia, ama mahali ulipoachia, na kuchukua kila Neno la Mungu.

¹⁸² Angalia tu jambo hilo kwenye huduma leo. Kama vile Balaamu alivyomwozesha kwenye kanisa la Mungu, kahaba, akamwoza kahaba kwenye kanisa la Mungu, vivyo hivyo ndivyo waalimu hawa wa uongo leo wanavyojaribu kuwaambia. Wao wataoza kila moja ya haya madhehebu na hawa watu kwa yule kahaba wa Ufunuo 17. Fundisho lao la Balaamu likizunguka leo, na kusema, “Sisi ni kitu kile kile tu. Sisi sote ni Wakristo.” Nao makasisi na mapapa, na wo wote wale, wote wakipatana na kufanya jambo hili.

¹⁸³ Yule mhubiri akasema; hata namjua mhubiri wa Kipentekoste, wote, wameanza sasa kutoa mkate mwembamba wa mviringo. Ambao unamaanisha, *Ashoteri*, “mungu mwezi,”

mkate mdogo mwembamba. Kasema, “Fungeni macho yenu mkaule, kama jambo hilo linaudhi dhamira zenu.” Fungeni macho yenu? Mkate mwembamba wa mviringo, unamaanisha nini? Tunakula mwili uliovunjwa-vunjwa, Yesu Kristo, aliyevunjwa; si mungu mwezi wa mviringo, Ashoteri, ambaye Mariamu alipachukua mahali pake. Na mkate mwembamba wa Kirumi ungali ni wa mviringo, kwa ajili ya mungu mwezi, mungu wa kike, si mungu. Tuna mkate uliovunjwa-vunjwa, bila shaka. Loo!

¹⁸⁴ Kwa hiyo sasa yule kahaba mkuu wa Ufunuo 17, hawa waalimu wa Balaamu na fundisho lao la uongo, wanalioza kanisa katika mchafuko kama huo. Angalia inapofikia kwenye lile shindano la mwisho wakati wa mwisho, angalia udhaifu wake sasa. Madhehebu mia tisa na kitu mbalimbali, moja likivuta njia moja, na lingine nyingine. Hakuna umoja kati yao. Nao wanajaribu kuleta umoja; usiyoungwa mkono na Neno la Mungu, mpango wa asili wa Mungu. Wao wanauingiza kwa siasa na madhehebu.

Mungu habadilishi nia Yake. Anakaa moja kwa moja na Neno Lake. Yeye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita.” Hiyo ni kweli. Yeye hudumu na Neno Lake la asili. Loo, jamani!

¹⁸⁵ Ingawa wao wangali wanahoji dhidi Yake, kama tu vile walivyofanya, na ninii tu... Kuna jambo moja tu la kufanya. Yeye hatalibadilisha Hilo. Aminini tu. Kwa kuwa, mbingu na nchi zitapita; Neno Lake halitashindwa kamwe. Mnaona?

¹⁸⁶ Mnaona mahali ambapo mnaozwa? Mnaona siasa na kadhalika, jinsi wanavyojaribu kuunganisha kanisa pamoja kwa siasa kanisani? Sisi hatuunganishwi na Kristo kwa siasa.

Tunaunganishwa, Kanisa, kwa Kristo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na namna unavyojua ubatizo wa Roho Mtakatifu, ni kwa kuwa Roho huyo ndani yako hutambua kila Neno la Mungu kwamba ni Kweli. Hiyo ni kweli. “Kwa kuwa mtu ye yote atakayeondoa neno moja kutoka Kwacho, wala kuongeza Neno moja Kwacho, sehemu yake itaondolewa kwenye Kitabu cha Uzima.”

¹⁸⁷ Hata hivyo, “Yeye anafanikiwa,” unasema. Huwezi kuamini Hilo kwa ufanisi. Huwezi kumpima Mungu kwa ufanisi. Ulimwengu hufanikiwa. Balaamu alifanikiwa kwake.

Bali, ndugu, unampima Mungu kwa Neno Lake. Yeye hudumisha Neno Lake na kulitambulisha kwamba ni Kweli. Kwa hiyo kumbuka, ewe rafiki, mradi ungali hai, usisahau jambo hili kamwe, Mungu habadilishi nia Yake. Hata hivyo, atabariki. Atakuacha uende kwa mapenzi Yake ya kuruhusia, bali Yeye hatabadilisha nia Yake. Hatabadilisha mpango Wake. Hatabadilisha Neno Lake, kwa ajili yako. La, bwana.

Huna budi kubadilika. Huwezi kulifanya Neno la Mungu lilingane na maisha yako; inakupasa kuyalinganisha maisha yako na Neno la Mungu. Unaona? Hivyo ndivyo unavyopaswa...

Unasema, “Vema, mimi ni mtu mzuri. Mungu hufanya jambo *hili, lile*, au *linginelo*.” Lakini wewe unalishika Neno Lake? “Loo, vema, nakwambia, hilo si ninii tu... Naam.” Sawa, kuna kasoro mahali fulani. Mungu ataninii... Naam, Yeye atakufanikisha. Hakika, atakufanya...

¹⁸⁸ Madhehebu yanafanikiwa kwa yeye ambaye asingelikuwa nayo! Wao wanapanua hema zao, makanisa makuu na mazuri, na kila kitu, kila mahali nchini. Wao ni matajiri, na pesa zinamiminikia mle, na wafuasi kutoka kila mahali. Si Biblia ilisema, “Ndani yake mlionekana hata utajiri wa ulimwengu, na hata roho za wanadamu,” na kila kitu, ambacho kilikutwa katika kahaba huyu wa kale, ambaye ni mama wa kitu hicho chote, siasa na madhehebu?

¹⁸⁹ Bali kundi dogo la Mungu ni Bibi-arusi Wake, moyo wake uko kwenye Neno hilo. Baba mpenzi wa Mbinguni na awaimarishe papo hapo daima. Msiondoke kamwe kwenye Neno hilo.

Unaweza kubariki, unaweza... Huenda Mungu akamponya mgonjwa wako. Huenda Yeye akamponya mtoto wako mchanga aliye mgonjwa. Huenda akamponya mume wako, mke wako. Huenda akamponya mama yako, mtu mwingine. Unaweza kuruka kwa Roho Wake, na kucheza ukirukaruka.

Kumbuka, mvua hunyea wenye haki na wasio haki, vivyo hivyo tu. Bali wakati hiyo mbegu imekaa pale, aidha imechaguliwa ama haijachaguliwa. Na iwapo imechaguliwa, inaweza... Kama ni ngano, haina budi kuzaa ngano. Kama ni Neno la Mungu, haina budi kuzaa Neno la Mungu. Kama sivyo ilivyo, vema basi sivyo ilivyo. Mnaona? Mnalielewa hilo sasa?

¹⁹⁰ Bwana awabariki. Hapa niliwaambia ningefunga kwenye saa tatu, na hii hapa, saa nne kasoro dakika kumi. Wengi wenu ninii watu, mna safari ndefu. Ninawapenda. Na sababu ya kuwachelewesha namna hii, si kwamba ninataka kuwa mkatili kwenu, bali ninawapenda. Na nijuavyo mimi, siwafichi kitu; mimi huwaambia Kweli.

¹⁹¹ Kule nje kwenye mikutano ninakoenda, hamnisikii nikihubiri Jumbe hizi. La, niliwaahidi, kuja kwenye Maskani hii. Papa hapa ndipo mimi huhubiria jumbe zangu. Nina tatu ama nne zaidi hapa, ambazo Bwana amenipa mimi, nina Maandiko juu yake, ambayo nisingethubutu kuhubiri mahali pengine po pote ila papa hapa. Hapa ndipo Neno la Mungu lilipoanzia. Na, hata Mungu atakapolibadili, ninakaa papa hapa na kuutoa papa hapa. Hiyo ni kweli.

Kule nje mikutanoni, nawaombea wagonjwa, na kila kitu namna hiyo; na, kando kando, nasema mambo kwa njia isiyo dhahiri, ambayo kondoo husikia. Wanajua kile kinachonenwa. Ama kweli, ni chambo tu kwenye ndoana, mnaona. Mimi huonyesha zile ishara za—za kujaribu kuonyesha ya kwamba Mungu anajua, katika utambuzi, na anajua mioyo ya watu, na hufanya mambo haya. Hicho ni kipawa cha kiinjilisti, kuwachochea tu watu.

Muda si muda, kanda inaangukia nyumbani mwao. Imelenga penyewe, basi. Kama yeye ni kondoo, anakuja moja kwa moja Nalo. Kama yeye ni mbuzi, anapiga hiyo kanda teke. A-ha. [Ndugu Ben Bryant anasema, “Nawe, pia.”—Mh.] Unaona, hiyo ni . . . “Nawe, pia,” ni kweli, Ben. Hiyo, hiyo ni kweli kabisa. Ben amekuwa na matukio fulani. Vema. Vema, hiyo ni kweli.

¹⁹² Hivi hamna furaha ya kwamba ninyi ni Wake? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivi hamna furaha? [“Amina.”] Tulizoea kuimba wimbo mdogo wa Kipentekoste, muda mrefu, kama:

Nina furaha sana ya kwamba Bwana alinitoa;
 Nina furaha sana ya kwamba Bwana alinitoa;
 Kama isingekuwa Yesu, ningekuwa wapi?
 Nina furaha sana ya kwamba Bwana alinitoa.
 Loo, nimekuwa na furaha tangu Bwana aliponitoe;
 Nimekuwa na furaha tangu Bwana aliponitoe;
 Kama isingekuwa Yesu, ningekuwa wapi?
 Nina furaha sana tangu Bwana aliponitoe.
 Nimekuwa nikipaza sauti tangu Bwana aliponitoe;
 Nimekuwa nikipaza sauti tangu Bwana aliponitoe.
 Kama isingekuwa Yesu, loo, ningekuwa wapi?
 Nina furaha sana ya kwamba Bwana alinitoa.

Utukufu! Hivi hamna furaha? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Hivi hamna furaha . . .” Na tuuimbe.

Hivi hamna furaha ya kwamba Bwana aliwatoa?
 Hivi hamna furaha ya kwamba Bwana aliwatoa?
 Kama isingekuwa Yesu, loo, ningekuwa wapi?
 Nina furaha sana ya kwamba Bwana alinitoa.
 Vema, nimekuwa nikiimba tangu Bwana aliponitoe;
 Nimekuwa nikiimba tangu Bwana aliponitoe;
 Kama isingekuwa Yesu, loo, ningekuwa wapi?
 Nina furaha sana ya kwamba Bwana alinitoa.

Hivi hamna furaha kwa ajili ya jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina.—Mh.] Basi, tutatembea Nuruni. Mnaujua wimbo huo?

Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri,
Hutokea ambako matone ya umande wa neema
yanang'aa;
Angaza kote kutuzunguka usiku na mchana,
Loo, Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Hivi hamuupendi huo? Hebu tuuimbe tena.

Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri,
Hutokea ambako matone ya umande wa neema
yanang'aa;
Angaza kote kutuzunguka usiku na mchana,
Loo, Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Ni kuchomoza kwa jua!

Enyi watakatifu wote wa Nuru tangazeni,
Yesu, Nuru ya ulimwengu;
Kweli na rehema katika Jina Lake,
Yesu, Nuru ya . . .

Sasa na tuinue mikono yetu tunapouimba.

Loo, tutatembea katika Nuru hii, ni Nuru nzuri
sana,
Hutokea ambako matone ya umande wa neema
yanang'aa;
Angaza kote kutuzunguka usiku na mchana,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Peaneni mikono mmoja kwa mwingine.

Loo, hutokea ambako matone ya umande wa
neema yanang'aa.

Hivi hamfurahi ninyi ni watoto wa Nuru? Mwana amechomoza.

. . .kutuzunguka mchana na usiku,

"Enyi watoto wadogo, pendaneni."

. . .Nuru ya ulimwengu.

Loo, tutatembea tu Nuruni, Ni Nuru nzuri
sa- . . . (kudhihirishwa kwa Neno Lake)
Hutokea ambako matone ya umande wa neema
yanang'aa,
Angaza tu kote kutuzunguka usiku na mchana,
Ni Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Nyote mnaamini jambo hilo?

Twenenda Sayuni.
 Mji mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

Loo, twenenda Sayuni.
 Mji mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

Wasiimbe wao
 Wasioamini;
 Watoto wa Mungu ndio
 Watoto wa Mungu ndio
 Waimbao chini,
 Waimbao chini.

Kwa kuwa twenenda . . . (Utukufu!)
 Mji mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

Loo, twenenda Sayuni.
 Loo, mji mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

¹⁹³ Toeni lesu zenu. Toeni lesu zenu, kwa muda kidogo. Na tumpe Bwana sadaka ya kutikisa. Si mganda, bali wao walitoa kwenye mwili wa Paulo lesu na kadhalika, mnaona.

Loo, twenenda Sayuni.
 Loo, mji mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

Loo, twenenda Sayuni.
 Loo, mji mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

¹⁹⁴ Amina! Loo, huo hauwafanyi kujisikia vizuri? Naweza tu kuwawazia hao watakatifu wa kale nyuma kule, kabla ya kuingia kwenye kile kiwanja cha tamasha cha Kirumi kule, wakianza kupanda kilima kile, mwajua, kupanda kile kipandio kidogo, wakupanda kuingia kwenye tundu la simba, wakisema:

Loo, twenenda Sayuni.
 Mji huu mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

Twaona rohoni
 Baraka za Mungu
 Tusijafika Mbinguni,
 Tusijafika Mbinguni,
 Kwenye utukufu,
 Kwenye utukufu.
 Twenenda Sayuni.
 Mji huu mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

¹⁹⁵ Semeni nyuma yangu. Bwana Mungu, [Kusanyiko linasema, “Bwana Mungu,”—Mh.] Ninajitolea mwenyewe upya Kwako. [“Ninajitolea mwenyewe upya Kwako.”] Nisafishe na uovu wote. [“Nisafishe na uovu wote.”] Nisafishe na mashaka yote katika Neno Lako. [“Nisafishe na mashaka yote katika Neno Lako.”] Nijalie, tangu Pasaka hii, [“Nijalie, tangu Pasaka hii,”] niwe kiumbe kipya [“niwe kiumbe kipya”] katika Kristo Yesu. [“katika Kristo Yesu.”] Nijalie nichukue, moyoni mwangu, [“Nijalie nichukue, moyoni mwangu,”] Neno Lako. [“Neno Lako.”] Na liwe Taa kwenye miguu yangu [“Na liwe Taa kwenye miguu yangu”] itakayoiangazia njia yangu. [“itakayoiangazia njia yangu.”] Tangu sasa, [“Tangu sasa,”] nitakufuata Wewe. [“nitakufuata Wewe.”] Katika Jina la Yesu. [“Katika Jina la Yesu.”] Amina. [“Amina.”]

Twenenda Sayuni.
 Loo, Mji huu mzuri Sayuni;
 Twenenda juu Sayuni,
 Ni Maskani ya Mungu.

¹⁹⁶ Hivi huo hauwafanyi kujisikia vizuri? [Kusanyiko linasema, “Amina.—Mh.] Tumejitolea wenyewe upya, tukijua ya kwamba mioyoni mwetu tumehuishwa kutoka mautini, tukafanywa hai. Hivi hilo haliwafanyi kujisikia vizuri? [“Amina.”] Jamani, loo, jamani! Ninawapenda, kwa upendo usiokufa.

Sikilizeni. “Pendaneni. Kwa kuwa huwezi kumchukia ndugu yako, ambaye unamwona, kisha useme unampenda Mungu, Ambaye hujamwona.” Mnaona? Kwa hiyo pendaneni tu.

Halafu, mnapotumikiana, mnamtumikia Mungu. Sivyo? “Mnapomtendea aliye mdogo sana wa hawa walio na Nguvu za Kuhuisha ndani yao, mmenitendea Mimi.”

“Tulikuona lini ukiwa mhitaji? Tulikutembelea lini gerezani? Tulitenda lini mambo haya?”

“Mliyowatendea hao, mlinitendea Mimi.”

¹⁹⁷ Si hilo ni la ajabu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ninampenda, nanyi je? [“Amina.”]

¹⁹⁸ Loo, kuna wimbo mmoja zaidi hatuna budi kuuimba, kama mna dakika moja zaidi. Loo, vema, tutawachukua tu. Vema.

Vema, bwana. Loo! *Peleka Jina La Yesu*. Msisahau jambo hilo, marafiki. Hebu sote tuuimbe sasa. Kila mmoja, pamoja sasa, tukiwa tu na moyo mmoja mkubwa, tuuchukue Kwake. Hebu, kwa yote tuliyo nayo ndani yetu.

Peleka Jina la Yesu,
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.

¹⁹⁹ Kumbukeni sasa, niombeeni wakati pepo za mateso makali zinapovuma, wakati pepo katika kila upande wanasai, nitakumbuka mnanionbea usiku ama mchana, nami nitakuwa nikiwaombea.

Muungeni mkono mchungaji wenu mwema, Ndugu Neville, na mwenziwe msaidizi, Ndugu Capps. Wasikilizeni. Wao watawafundisha Neno la Uzima. Ninaamini jambo hilo. Kama nisingaliliamini, bila shaka nisingaliwaleta hapa. Bila shaka nisingaliwaleta. Ninaamini ya kwamba wao wanaamini Ujumbe, nao wanadumu nao vizuri wajuavyo, nami nina imani katika watu hao wawili. Kaeni nao. Hawa ndugu wengine, karibu sehemu zile wanakofanya mikutano yao, waliosimama hapa usiku huu, kama mkiwa karibu na waliko, waungeni mkono. Mlisikia kilichowaleta hapa, usiku huu.

Peleka Jina la Yesu,
Ko kote uendako; (sikilizeni jambo hili)
Utakapojaribiwa,
Lilia Jina hilo.

Thamani, thamani, na tamu! na tamu!
Ni Jina . . .

Mungu mpendwa, waponye watu hawa. Ninakuomba Wewe, Baba, katika Jina la Yesu. Tujalie, Bwana, naomba.

. . . na tamu!
Ni Jina Lake Yesu
Hata twonane huko juu!
Hata twonane Kwake kwema;
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Mungu Awe Nanyi*—Mh.] Ee Mungu, uwe pamoja nasi. Tusaidie, Bwana.

. . . twonane Kwake kwema! (Kwake kwema!)
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

²⁰⁰ Hilo kweli ndilo ombi langu. Hata twonane tena, Mungu awabariki! Na sasa nitamwomba Ndugu yetu mpendwa Neville kama angeruhusu kusanyiko hili zuri lifumukane.

Mungu anawapenda, kila mmoja. Nina furaha sana kuwa na watu kama ninyi nyote. Ujumbe wangu ungekuwa nini kama nisingalikuwa na mtu aliyeuamini? Na kuna watu hapa, mngékufa kwa ajili Yake, kwa ajili ya Ujumbe huu. Mungu na awasaidie, kila mmoja. Maombi yangu yako pamoja nanyi. Baraka zangu ziambatane na kila mmoja wenu. Naomba msisahau ya kwamba ninyi ni sehemu ya ufufuo ule. Zile Nguvu za Kuhuisha zimo sasa ndani yenu. Yote yamekwisha. Wewe ni mtoto wa Mungu.

Na tuinamishe vichwa vyetu, hata Ndugu Neville atakapoturuhusu. Basi Mungu awabariki.



JE! MUNGU HABADILISHA NIA YAKE KUHUSU NENO LAKE? SWA65-0418E
(Does God Ever Change His Mind About His Word?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Aprili 18, 1965, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1996 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org